

**BILA MISSO MISONDO HUJAMALIZA 2023**

UKURASA 11

**WANANCHI** waomba elimu kutambua vifungashio vyenye dawa za kulevya

UKURASA 8



**VIONGOZI** makanisa DRC wabaini kasoro kwenye uchaguzi

UKURASA 17




# Nipashe

Jumamosi Desemba 30, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581540

www.ippmedia.com

LIKE & FOLLOW US

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper


# SHAMBULIO LA MAUAJI ROMBO

**POLISI** yamsaka mtuhumiwa, atoweka baada ya...

*Endelea ukurasa wa 2*





UKURASA WA 8

## KAYA 119 ZILIZOKUMBWA MAFURIKO MOSHI ZAKUMBUKWA

SERIKALI imetoa misaada ya vyakula, magodoro, ndoo, madumu na mablanketi kwa kaya 119 zilizoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro zilizokumbwa...

UKURASA WA 17

## WAPALESTINA NI PURUKUSHANI USIKU NA MCHANA KUJIOKOA

WAKATI vikosi vya Jeshi la Israel vikizidi kusonga mbele katikati ya ukanda wa Gaza, jumla ya Wapalestina 150,000 wanatakiwa kuondoka...



UKURASA WA 20

## AZAM FC: TUMEJIRIDHISHA UWEZO WA NAVARRO

UONGOZI wa Klabu ya Azam FC umesema ulimfuatilia kwa kina na kujiridhisha uwezo alionao mchezaji wao mpya Franklin Navarro na kuamua kumsajili...



UKURASA WA 24

## YANGA YATOA SABABU KUMSAJILI OKRAH

UONGOZI wa Klabu ya Yanga umesema ulimfuatilia winga wa Ghana, Augustine Okrah na kuona anafaa kwenye kikosi chao na hivyo kuamua kumsajili ili kukiongezea nguvu....



## Wanandoa kortini tuhuma usafirishaji dawa za kulevya

UKURASA 3



## Malaria tishio, yaua 36 Zanzibar

UKURASA 10

**MICHEZO** SIMBA YATAKA REKODI MAPINDUZI CUP UK. 24 **KATUNI** UK. 6



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Simon Maigwa

Beatrice James Minja (47) mkazi wa Tarakea, Rombo, wakati akiwa hospitalini kabla ya umauti kumkuta. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shambulio la mauaji Rombo, polisi yamsaka mtuhumiwa

## ●Prof. Mkenda aonya upotoshaji taarifa mitandao kijamii...

**Na Godfrey Mushi,** ROMBO

NI tukio la kinyama na mwendelezo wa ukatili dhidi ya wanawake baada ya Beatrice Minja (47), kuuawa kwa kuchomwa visu mara 25 na anayedaiwa kuwa mpenzi wake, Lucas Tarimo.

Mkasa huo ulioteka hisia za watu wengi kwenye mitandao ya kijamii nchini, ulitokea Novemba 12, mwaka huu, baada ya mwanamke huyo alipodaiwa kushambuliwa na mtuhumiwa huyo.

Baada ya shambulio hilo, Beatrice ambaye ni mkazi wa Tarakea, Wilaya ya Rombo, mkoani Kilimanjaro, alikimbizwa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC iliyoko Moshi na kupatiwa matibabu, lakini alifariki dunia siku tatu zilizopita (Desemba 27, mwaka huu). Mtuhumiwa bado hajulikani aliko.

Wakati tukio hilo likitikisa, Msemaji wa Jeshi la Polisi Nchini (SACP), David Misime, alisema jana kuwa, jeshi hilo limeona taarifa hiyo ikizagaa katika mitandao ya kijamii huku kumbukumbu zao zikionyesha lilitokea na kuripotiwa polisi, Novemba 12, mwaka huu.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari, Misime alisema mwanamke huyo alipoteza maisha Desemba 27, mwaka huu, wakati akiendelea na matibabu katika Hospitali ya KCMC.

Misime alisema baada ya tukio hilo, taratibu za ufuatiliaji zilianza kwa kupata maelezo ya wanawake waliokuwa na Beatrice siku ya tukio, ikiwa ni pamoja na kumtafuta mtuhumiwa ambaye alikimbia baada ya kutenda uhalifu huo.

"Jeshi la Polisi linaendelea kumsaka mtuhumiwa ambaye jina lake halisi ni Lucas Tarimo maarufu Tarimo, ambaye shughuli zake ni fundi wa nyumba anazofanya katika maeneo mbalimbali.

"Tunamsaka ili akamatwe na taratibu nyingine za kisheria zifuate, kwani hakuna aliye juu ya sheria hata kama ana nafasi gani katika jamii au taifa.

Misime alisema Jeshi la Polisi linatoa rai kwa yeyote atakayemwona mtuhumiwa huyo asisite kutoa taarifa ili akamatwe.

Pia, alisema wanatahadharisha kwa yeyote ambaye anamficha au anamsaidia kuendelea kujificha, akibainika hatua zitachukuliwa dhidi yake kwa mujibu wa sheria.

"Tukio hili limemtokea binadamu na Mtanzania mwenzetu, ni la kusikitisha na la kulaaniwa. Tunasihi mwenye taarifa sahihi hata kama kuna uzembe mahali, tutashukuru akitufikishia ili zifanyiwe kazi.

Misime alisema Jeshi la Polisi linawataka wananchi kujiepusha na taarifa za uzushi na uongo zenye malengo ya kuchafua watu wengine kwa nia binafsi.

**MKENDA AONYA**

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, ambaye ni Mbunge wa Rombo, amehadharisha wanaojaribu kumchafua kisiasa kwa kutumia tukio hilo kuwa wanajishusha kwenye matope kwa kina cha chini.

"Ukweli ni kwamba, ninajua polisi wanafanya kazi usiku na mchana kumsaka mtuhumiwa wa mauaji haya. Ninajua kwa vile na mimi ninafuatilia kwa karibu sana.

"Naungana na watu wote kulaani kwa nguvu zote mauaji haya ya kikatili sana. Lakini vilevile, ningeomba watu wanaoandika kwenye mitandao, hasa wale ambao wameshajijengea imani kwa watu, kuhakiki taarifa wanazozitoa kabla ya kutuma kwenye mitandao ya kijamii.

"Kwa mfano, yuko bwana maarufu sana kwenye mitandao na watu wengi wanamwamini. Ameandika kwamba mtuhumiwa wa mauaji haya ni mfanyakazi wa nyumbani kwangu, mimi Mbunge wa Rombo.

"Taarifa hizi si sahihi kabisa na hata angekuwa mfanyakazi nyumbani kwangu, hakuwezi kumwondolea mtuhumiwa suala la kukamatwa, kushtakiwa kwa mauaji haya," alisema.

Hata hivyo, Prof. Mkenda alisema kufanya kazi nyumbani kwa mbunge, si kinga dhidi ya uharamia, hivyo uhalifu huo mkubwa ni wa kulaaniwa kwa nguvu zote.

Prof. Mkenda alikanusha tuhuma kwamba mtuhumiwa huyo anafanya kazi nyumbani kwake.

"Na mimi japo nalifuatilia suala hili kwa karibu, sio kwenda kwenye social media (mitandao ya kijamii) ninafuatilia kwenye vyombo vya ulinzi na usalama, ninajua huyu bwana aliyepost (aliyechapisha) kwamba mtuhumiwa ni mfanyakazi wa nyumbani kwangu, hata jina alililoandika si sahihi.

"Kwa heshima yake, ninamwomba aondoe taarifa hii na mbele ya safari ajifunze kuhakiki taarifa nyeti kama hizi kabla ya kuanza kuzisambaza, kwa sababu akiendelea hivi, hata wale wanaomwamini watapungua kutokana na kuona anakurupuka kutoa taarifa ambazo hajazihakiki na kuzisambaza.

Prof. Mkenda alisema anaungana na watu wote kulaani mauaji hayo ya kinyama na kwamba, anaamini mtuhumiwa atakamatwa na kufikishwa mbele ya vyombo vya sheria na haki itachukua mkondo wake.

"Lakini tujaribu sisi wengine kuondoa siasa kama una nia ya kumchafua mtu kwa kutumia mauaji ya ndugu yetu Beatrice Minja, hiyo ni kujishusha kwenye matope kwa kina cha chini sana," alionya.

Kadhalika, taarifa zilizosambaa mtandaoni zilidai mtuhumiwa wa mauaji hayo kabla ya kutoroka baada ya tukio hilo, alimpora Beatrice Sh. milioni 10, ambazo zilikuwa mtaji wa biashara pamoja na fedha za ujenzi wa nyumba ya mama yake.

HABARI KITAIFA

# Zaidi ya vijana 5,000 wapatiwa mafunzo ujasiriamali

**Na Sabato Kasika**

KITUO cha Sauti ya Jamii Kipunguni jijini Dar es Salaam, kimetoa mafunzo ya ujasiriamali kwa watu 5,842 katika kipindi cha miaka minane.

Mafunzo hayo ni ya mapishi, kilimo rahisi, jinsi ya kusimamia vikundi, saluni, utengenezaji wa urembo na mkaa mbadala na jinsi ya kuanzisha klabu za kupinga ukatili.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana wakati akielezea tathmini ya shughuli zilizofanywa na kituo hicho kwa miaka hiyo, Mkurugenzi wa kituo hicho, Seleman Bishagazi, alisema mafunzo hayo ni sehemu ndogo ya wanachofanya ndani ya jamii.

Alisema kwa kipindi hicho chote, wanawake waliopata mafunzo ni 2,100, wanaume 510, vijana wa kike 2,700, wa kiume 300, wenye ulemavu wa kike 161 na wa kiume 71, ambao jumla yao ni 5,842.

Akizungumzia klabu za kupinga ukatili wa kijinsia kwa upande wa watoto, alisema zipo 30, vijana 30, za wazazi 30, mabinti wenye watoto 30 ambazo idadi yake kamili ni 120.

"Tunafanya kazi nyingi tukijikita zaidi kupambana na ukeketaji na ukatili wote kwa ujumla, lakini ndani ya kazi hiyo tunaipa jamii elimu ya kuachana na vitendo hivyo na njia mbadala ya kujipatia kipato badala ya kutegemea ukeketaji ambao kimsingi haukubaliki," alisema Bishagazi.

Alisema katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilala, kituo chao kimekuwa kikitolewa kama mfano kuwa kinafaa kuigwa kutokana na shughuli ambazo kinafanya ndani ya jamii za kupambana na ukeketaji.

"Kipunguni na maeneo mengine ya huku kuna ukeketaji mwingi, wanafanya hivyo ili kujipatia kipato, nasi tunawahamisha kutoka kwenye mawazo hayo, ili wafanye shughuli nyingi halali, lakini pia sheria ikichukua mkondo wake," alisema.

Bishagazi alisema, hatua ya serikali kutambua shughuli za kituo hicho ni ya kinajivunia hilo na kwamba wanatumia nafasi hiyo kuendelea kufanya kazi kubwa zaidi ya kupambana na ukeketaji.

"Tulipata mafunzo kupitia semina za Jinsia na Maendeleo za Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) na tumeamua kujenga ofisi yenye thamani ya Sh. milioni 11 kupitia vyanzo vyetu vya mapato na sasa inatoa msaada wa kisheria, jamii inapata huduma hiyo kwa karibu.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii wa Jiji la Dar es Salaam, Francisca Makoye, alisema Ilala kuna vikundi vingi, kimojawapo kinachofanya vizuri kikiwa ni Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni.

Alisema, katika vikundi vilivyopo Ilala, Sauti ya Jamii Kipunguni cha Kata ya Kipunguni, kimeimarika na kujikita katika shughuli za ujasiriamali na hatua hiyo inakwenda sambamba na kutatua changamoto zinazotokana na ukatili wa kijinsia kwa watoto na wanawake.

"Kituo hicho kinafaa kuwa mfano wa kuigwa katika vita dhidi ya ukatili wa kijinsia ndani ya jamii ili kuharakisha jitihada za kukomesha vitendo hivyo nchini," alisema Francisca.

Alifafanua kuwa kimewezesha jamii ya kata hiyo na za jirani za Kitunda na Kivule kufanya shughuli za kiuchumi na kuanzisha klabu za watoto ili kuwalinda dhidi ya vitendo vya ukatili na kuwaendeleza.

# Wanandoa kortini watuhumiwa kusafirisha dawa za kulevya

**Na Kulwa Mzee**

MKAZI wa Kibugumo Kigamboni, Najim Mohamed, mke wake Maryam Mohammed na mfanyakazi wa ndani, Juma Abbas, wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kwa tuhuma za kusafirisha dawa za kulevya, kilogramu 3,050.

Mohamed, Maryam (50) na Abbas (37), walipanda kizimbani jana na kusomewa mashtaka mawili yanayowakabili mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Aaron Lyamuya.

Akisoma mashtaka hayo Wakili wa Serikali Hemed Halfani akishirikiana na Frank Michael, alidai washtakiwa walitenda kosa Desemba 15, 2023 eneo la Kibugumo Shule, Wilaya ya Kigamboni, wanadaiwa kusafirisha Heroine kilogramu 882.71.

Katika shtaka la pili, siku na eneo hilo, washtakiwa kwa pamoja wanadaiwa kusafirisha dawa za kulevya aina ya Methamphetamine kilogramu 2167.29.

Baada ya kusomewa mashtaka washtakiwa hawakutakiwa kujibu, Hakimu Lyamuya alisema hawatakiwi kujibu chochote mahakamani hapo kwa kuwa mahakama hiyo haina uwezo wa kusikiliza kesi za uhujumu uchumi.

Upande wa Jamhuri ulidai upelelezi wa shauri hilo haujakamilika na kesi imeahirishwa hadi Januari 11, 2024 itakapotajwa na washtakiwa wamerudishwa rumande.



Katapila likisawazisha barabara eneo la Rest House lililoko Kata ya Kisemo, Tarafa ya Matombo, Wilaya ya Morogoro Vijijini, mkoani Morogoro ambalo ni maarufu kwa magari kukwama. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Neema Tabora, yakabidhiwa magari mawili ya wagonjwa

**Na Benny Kingson,** TABORA

SERIKALI imeikabidhi Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tabora Kitete magari mawili ya wagonjwa, moja likiwa na uwezo wa kutoa huduma za matibabu ya dharura wakati mgonjwa akiwahishwa hospitalini.

Magari hayo yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 100 yalikabidhiwa kwa uongozi wa hospitali hiyo na Mbunge wa Tabora Mjini, Emmanuel Mwakasaka na lingine ni kwa ajili ya utawala.

Mwakasaka alisema, amewapambania wakazi wa manispaa hiyo, mkoa na mikoa ya jirani kuhakikisha magari hayo muhimu yanapatikana ili kurahisisha utoaji wa huduma za afya kwa kuzingatia kuwa kulikuwa na upungufu huo.

"Rais Samia anatosha sana na ametushibisha na anaendelea kutushibisha. Hakuna shaka kwamba ukiondoa mikoa ya Dodoma na Dar es Salaam wamekuwa wakipatiwa fedha nyingi za miradi na sisi Tabora tunafuatia, kwani tumeletewa fedha za kutosha katika sekta mbalimbali," alisema.

Mganga Mkuu Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Mark Waziri, alisema ujio wa magari hayo hasa la wagonjwa utasaidia kurahisisha utoaji wa huduma zao na kupanua wigo wa utendaji kazi.

Dk. Waziri alisema wanahudumia wagonjwa wa rufani wapatao 278 na kutaja baadhi ya changamoto zinazowakabili ni mfumo wa majitaka unaotakiwa kuboreshwa na wa majisafi kuongezwa.

Akitoa taarifa kwa niaba ya Mganga Mkuu wa mkoa, Dk. Nassoro Kaponta, alisema wana vituo vya kutolea huduma za afya 406 kati yake hospitali ni 15, vituo vya afya 43, zahanati 341 na kliniki saba.

Alisema kati ya vituo 406 walivyonavyo, 343 sawa na asilimia 84 vinatoa huduma za kliniki ya wajawazito na watoto na 30 vinatoa huduma za upasuaji na damu huku idadi ya wakazi ikiwa ni 3,391,679 wakati kinamama wenye umri wa kuzaa wenye umri wa kati ya miaka 15 hadi 49 ni 791,379.

"Kwa kipindi cha Januari hadi Oktoba 2023, jumla ya kinamama 104,309 walijifungua kati yao, 101,856 sawa na asilimia 97 walijifungua katika vituo vya afya, 2,453 sawa na asilimia tatu walijifungua katika jamii, 1,507 walijifungulia njiani, 845 nyumbani na 101 kwa wakunga wa jadi," alisema.

Dk. Kaponta alisema kutokana na ukosefu wa magari ya kubeba wagonjwa inasababisha wajawazito kushindwa kufika kwenye vituo vya kutolea huduma za afya suala ambalo ni hatari kwa maisha ya mama na mtoto.




Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda, akizungumza katika ibada maalumu ya maombi kwa ajili ya Taifa na Rais Samia Suluhu Hassan ilioandaliwa na Kanisa la New Life Gospel Community Church lililoko Nyakato, Manispaa ya Musoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

MGOGORO HIFADHI/WANAKIJIJI

# Bil. 26/- za fidia zilizoahidiwa na serikali bado hazijatolewa

**Na Halfani Chusi**

FIDIA kwa wakazi wa Mbarali wanaopaswa kupisha Hifadhi ya Taifa Ruaha bado haijalipwa na serikali.

Rais Samia alielekeza Agosti 8, mwaka huu, akiwa mkoani Mbeya kwamba wananchi hao walipwe fidia na kupisha uhifadhi, akiahidi serikali kutoa Sh. bilioni 26 kwa ajili ya fidia hiyo.

Ni maelekezo yaliyotolewa na Mkuu wa Nchi kwa watendaji wa Wizara ya Fedha na Mkoa wa Mbeya baada ya kuwapo migogoro ya kimpaka kati ya wanakijiji na Hifadhi ya Taifa Ruaha.

"Nimepokea maombi kadhaa ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera. Anaomba fidia kule Mbarali na mshauri wangu wa siasa na mambo ya jamii kwa sababu aliwahi kuwa Waziri wa Ardhi, akaniletea tathmini ya fidia inayotakiwa pale.

"Nikaangalia na Waziri wa sasa wa Ardhi, idadi ni hiyo hiyo, Sh. bilioni 26. Sasa Mkuu wa Mkoa, mimi ninakwenda kutafuta hizi bilioni na pengine mapema mwezi ujao (Septemba) tunaweza tukaanza kulipa hizi fidia.

"Kwa hiyo, Waziri wa Ardhi na timu yako, mjipange ili tuweze kwenda kufanya hiyo kazi pale. Fidia Mbarali zinakwenda kulipwa, nitakwenda kuingia kwenye vikapu nichange huko mpaka zipatikane," aliahidi Rais Samia.

**UTEKELEZAJI**

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliiambia Nipashe juzi kuwa fedha za kulipa fidia hiyo hazijatolewa. Wanaendelea na tathmini.

"Tathmini ya kina inaendelea. Baada ya hapo watalipwa fedha zao. Kinachoendelea mpaka sasa ni kujiridhisha kwa kufanya uthamini wa kina ili kila mtu apate haki yake. Baada ya hapo tutalipa fidia na kuwahamisha," alisema.

Migogoro kati ya wanakijiji na Hifadhi ya Taifa Ruaha ilimlazimu Mtendaji Mkuu wa wa Shughuli za Serikali Bungeni, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa kuunda kamati ya kuchunguza na kurejea na mrejesho baada ya kuwasilishwa hoja bungeni kwamba baadhi ya wananchi waliteswa na askari wa hifadhi hiyo.

> **"Hakuna fidia iliyolipwa hadi sasa. Wananchi hawajalipwa mpaka leo (juzi). Kuna maeneo tathmini ilikuwa inafanyika, cha ajabu mpaka leo hakuna kinachoendelea.**

Kamati hiyo ilijumuisha viongozi wa serikali akiwamo Waziri wa Maliasili na Utalii, kipindi hicho, Mohamed Mchengerwa ambao mara moja walifika eneo la tukio kwa ajili ya kupata maelezo ya kina na kisha kurejea na majibu.

Golyama Masingija, mkazi wa Mbarali, katika mazungumzo na Nipashe juzi, aliomba serikali itimize ahadi yake ili wajue hatima yao na kuepuka alichokiita uhasama kati yao na askari wa hifadhi.

"Tulimsikia Rais, aliahidi serikali itatoa Sh. bilioni 26 ili tulipwe fidia na tuhamishwe. Tunasubiri, tupo tayari kuhama, lakini hatujui pa kwenda na mifukoni mwetu hamna kitu.

"Tunaiomba serikali kama ilivyoahidi itimize. Rais ni msikivu, ninaamini hili litaisha mapema sana," alisema Masingija.

Hawa Sengeje, alisema wanatamani walipwe fidia haraka ili watafute maeneo mengine watakakofanya shughuli.

"Watulipe fidia zetu, maana kuna maeneo walishakuja hata kufanya uthamini, lakini hawajarudi tena, hatujui kinachoendelea huko.

"Tunamwomba Mkuu wa Mkoa ajitahidi kutujuza kila kinachoendelea huko ngazi za juu. Hii itasaidia kupunguza maswali kwa wananchi," alisema.

Diwani wa Imalilo Songwe, Chuki Mbwanjine, uliko mgogoro huo, anaitaka serikali kuwajibika kwa wananchi kwa kuwapa taarifa ya kila hatua inayoendelea kuhusu suala hilo.

"Hakuna fidia iliyolipwa hadi sasa. Wananchi hawajalipwa mpaka leo (juzi). Kuna maeneo tathmini ilikuwa inafanyika, cha ajabu mpaka leo hakuna kinachoendelea.

"Shida ilikuja kutokana na GN 28, hili ni jiwe la mpaka kati yetu na Hifadhi ya Ruaha, linaonesha tupo ndani ya hifadhi wakati si kweli. Sisi mpaka wetu ulikuwa ni Mto Ruaha," alidai diwani huyo.

## Serikali kuendeleza msisitizo mazao chakula, biashara

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali imeweka msisitizo wa kuendeleza sekta mbalimbali nchini ikiwamo ya kilimo kwenye mazao ya chakula na biashara.

Amesema lengo ni kuhakikisha nchi inajitosheleza kwa chakula na kila Mtanzania anayejishughulisha na kilimo aweze kunufaika kwa kufanya biashara na kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza kwa nyakati tofauti na wananchi katika vijiji vya Litama, Chinongwe, Likwachu, Luchelegwa na Nandanga akiwa katika ziara ya kikazi wilayani Ruangwa, mkoani Lindi.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan amedhamiria Tanzania kuwa kimbilio la wengine wanaohitaji chakula.

"Tumuunge mkono Rais wetu kwenye mapambano yake ya kukuza sekta ya kilimo na amefanya makubwa kwenye sekta hii ikiwamo kuagiza kutengwa maeneo maalumu ya kilimo kwa ajili ya vijana, alisema.

Alisema licha ya serikali kuwa na mikakati ya kuimarisha sekta ya kilimo, pia imeendelea kuboresha sekta nyingine za afya, elimu, maji, umeme, miundombinu na biashara ili kuhakikisha wananchi katika maeneo mbalimbali nchini wanapata maendeleo.

Dhamira ya serikali ni kuhakikisha wananchi wote wanapata maendeleo kwa kuimarisha huduma za kijamii katika maeneo yote nchini yakiwamo ya Wilaya ya Ruangwa," alisema.

Akiwa katika Kijiji cha Chinongwe, alitembelea zahanati ya kijiji hicho ambayo miundombinu yake imefanyiwa maboresho na kumwagiza Mganga Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa kuongeza daktari mmoja ili kuboresha huduma.

Pia alimwagiza Ofisa Elimu wa Wilaya ya Ruangwa, kuwahamisha walimu kutoka kwenye shule zenye walimu wengi na kuwapeleka zenye upungufu ikiwamo Shule ya Msingi Litama yenye walimu wanne huku mahitaji yakiwa wanane.

Akizungumzia uboreshaji wa miundombinu, Waziri Mkuu alisema Rais Samia Suluhu Hassan, ameongeza bajeti TARURA kwa Wilaya ya Ruangwa imeongezeka kutoka Shilingi bilioni moja hadi Sh. bilioni 4.8, kwa ajili ya ujenzi na maboresho ya barabara za ndani na madaraja na kuwaomba wananchi waendelee kumuunga mkono.

# HABARI PICHA



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Ruangwa, akizungumza na Mwenyekiti wa Kijiji cha Juhudi B, Jafari Mnaheka, Kata ya Chinongwe, mkoani Lindi. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**



Mhifadhi Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Moronda Moronda, akipanda mti katika Kijiji cha Bukore, Kata ya Kunzugu wilayani Bunda, mkoani Mara, kwa ajili ya kuhifadhi mazingira. Hifadhi hiyo imetoa miche 13,000 kwa vikundi mbalimbali wilayani humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Ramadhan Ng'anzi (wa pili kushoto), akikagua pikipiki zilizokamatwa mjini Morogoro juzi, kwa makosa mbalimbali ikiwamo kubeba abiria zaidi ya mmoja. **PICHA: MPIGPICHA WETU**



Katibu wa UWT Wilaya ya Muheza, Tanga, Asnath Jeremia, akizungumza na wanachama pamoja viongozi wa jumuiya hiyo, jana kwenye kikao cha kawaida cha Baraza la UWT cha kufunga mwaka katika ukumbi wa Tate Plus. Mgeni rasmi alikuwa Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Theresia Ilet. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Barabara ya Mtaa wa Kamwela, Goba Matosa, ikiwa imeharibika kutokana na mvua inayoendelea kunyesha jijini Dar es Salaam na kusababisha usumbufu kwa wapita njia na madereva wa vyombo vya moto. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Mhifadhi wa Ujirani Mwema kutoka Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Robert Masobeji (kulia), akitoa maelezo kwa Mkuu wa Wilaya ya Serengeti, Fauzia Katumbura (kushoto) na timu yake kuhusu kutumia vifaa vya kufugia nyuki kama fursa ya kiuchumi kwa vikundi mbalimbali vya ujasiriamali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Maandalizi ya Stars, Twiga Stars AFCON isiachiwe TFF

FAINALI za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2023), zinatarajia kufanyika kuanzia Januari 13 hadi Februari 11, mwakani nchini Ivory Coast.

Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), imefanikiwa kufuzu fainali hizo, ikikata tiketi kwa mara ya tatu, mara ya kwanza ilikuwa ni mwaka 1980 michuano ikifanyika Nigeria, halafu ikashiriki tena mwaka 2019 huko Misri.

Pia Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), itashiriki fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wanawake (WAFCON 2024), ambazo zitafanyika Morocco kati ya Juni na Julai, mwakani.

Hii ni mara ya kwanza kwa Taifa Stars na Twiga Stars, zote zinashiriki fainali hizo, kwa kufika hatua hii, pongezi za awali zinatakiwa kuanzia kwa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), serikali na wachezaji kwa kujitoa kufika hapo.

TFF imekuwa karibu na serikali ya Dk. Samia Suluhu Hassan, kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhakikisha mambo yanakwenda sawa na kuendelea kuipa heshima Tanzania.

Siku zimebaki chache kabla ya kuanza kwa AFCON huko Ivory Coast na Taifa Stars iliyoko chini ya Kocha Mkuu, Adel Amrouche, imeshaanza maandalizi kwa ajili ya kuhakikisha kikosi kinaimarika na kinakuwa tayari kwa ajili ya kwenda kupeperusha vyema bendera ya Tanzania.

Ili wachezaji waende kupambana katika fainali hizo, ni lazima maandalizi yao yafanyike katika kiwango cha juu kwa sababu wanakwenda kushiriki michuano ya daraja la juu kwa timu za taifa hapa barani Afrika.

Kwa miaka mingi huko nyuma mashabiki wa soka wa Tanzania walikuwa wakishuhudia fainali hizo huku wakichagua mataifa ya kuwashangilia, kila mmoja kwa sababu zake, lakini mwakani hali itakuwa tofauti, wadau wa soka watafuatilia fainali hizo huku wakisubiri kuona wawakilishi wao wakipambana.

Ili kupata matokeo chanya, mbali na ubora wa wachezaji, timu hiyo inahitaji fedha kwa ajili ya kupatiwa mahitaji mbalimbali ikiwamo usafiri wa ndege, vifaa vya michezo vyenye ubora bila kusahau posho za wachezaji na viongozi wa benchi la ufundi.

Lakini pia inahitaji kuweka kambi mahali ambapo benchi la ufundi na TFF inaamini patasaidia kukijenga kikosi kuelekea michuano hiyo inayosubiriwa na wadau mbalimbali wa soka duniani, lakini haya yote hayatawezekana kama fedha zinazohitajika zitakosekana.

Miaka ya nyuma tulizoea kuona Stars ikitumia zaidi ya mwezi mmoja kukaa kambini kwa ajili ya kufanya maandalizi ya kushiriki michuano mbalimbali, lakini kwa sasa hilo haliwezekani kutokana na kikosi kuundwa na idadi kubwa ya wachezaji wanaocheza ughaibuni, kwa maana hiyo kanuni za FIFA hapo zinatumika kwa kuwapata nyota walioitwa kwa muda mfupi.

Kwa upande wa Twiga Stars, muda wa kuwapeleka kambini ughaibuni ili kuwaimarisha unaweza kupatikana, hii ifanyike kwa malengo ya kuwaongezea uzoefu wachezaji wetu kwa sababu tunaamini, popote watakapokwenda kujifua, watapata michezo ya kirafiki ya kimataifa ambayo itawaongezea ujuzi.


Tuliona kilichotokea kwa Serengeti Girls, serikali iliipeleka England kuweka kambi na matokeo yake yalionekana kwa wawakilishi hao wa Tanzania kufika hatua ya robo fainali.

Huu ndio muda wa kampuni na taasisi mbalimbali kujitokeza kuidhamini na kuichangia Taifa Stars pamoja na Twiga Stars, ili timu zetu ziende AFCON na WAFCON kushindana na si kusindikiza mataifa mengine.

Wadau tunatakiwa tushiriki katika maandalizi ili kuwa na timu imara na tusisubiri kutoa ahadi za ushindi au kununua mabao wakati fainali hizo zitakapoanza.

Kila la heri Taifa Stars, kila la heri Twiga Stars.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






**Muungwana Lazima Nilonge**

Na Adam Fungamwango

## Mapinduzi Cup ikiboreshwa, kubeba hadhi ya Kagame Cup

**TULIANZA** kuona sherehe za ufunguzi wa Uwanja wa Amaan, Zanzibar zilizofanyika Desemba 27, mwaka huu zilivyofana.

Wasanii kadhaa akiwamo Diamond Platnumz walitumbuiza, jukwaani kukiwa na wageni mbalimbali waalikwa waliokuwa chini ya mgeni rasmi, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Na siku hiyo timu mbili za Tanzania zilikuwa zinacheza, mwenyeji Zanzibar (Zanzibar Heroes), waliwakaribisha ndugu zao kutoka Tanzania Bara (Kilimanjaro Stars), katika mechi ya kirafiki iliyomalizika kwa suluhu.

Kesho yake kukakatwa utepe wa mashindano ya Kombe la Mapinduzi ambayo yanashirikisha timu 12 kutoka ndani na nje ya Tanzania.

Kundi A lina timu za Azam FC kutoka Dar es Salaam, Chipukizi United, Mlandege zote za Zanzibar na Vital'O ya Burundi wakati Kundi B linaundwa na JKU ya Zanzibar, Simba (Dar es Salaam), Singida Fountain Gate (Singida) na APR kutoka Rwanda wakati Yanga (Dar es Salaam), Jamus (Sudan Kusini) na Jamhuri ya Zanzibar wanaunda Kundi C.

Tangu kuingia kwa Dk. Mwinyi madarakani tumeanza kuona michuano ya Kombe la Mapinduzi ikizidi kuongeza umaarufu na msisimuko.

Siyo kama huko nyuma haikuwa hivyo, awali miaka ya nyuma ilikuwa na msisimuko mkubwa zaidi kuliko hata leo, lakini hapa katikati kulizuka 'upepo' fulani ambao uliifanya michuano hiyo kama ya kwenda kupoteza muda.

Hapo ndipo tukaanza kuona Simba na Yanga zikipeleka vikosi vya vijana chini ya miaka 20 na kuifanya izidi kukosa ule msisimko wake wa miaka ya nyuma.

Viongozi wa klabu hizi kubwa ambazo zinatazamiwa kwenda kuleta chachu walianza kupeleka watoto, badala ya vikosi vyao vya wakubwa.

Tena afadhali wangekuwa wanapeleka wachezaji ambao hawapati nafasi kwenye vikosi vyao, walikuwa wanapeleka wale wa timu za vijana kabisa kitu ambacho kilianza kupigiwa kelele na mashabiki wengi wa soka.Jambo hili sasa likaanza kuingiliwa si na viongozi wa soka Zanzibar tu ambao walionekana kushindwa, bali hata viongozi wa ngazi za juu, nadhani baadaye likawekwa sawa.

Kwa miaka michache hii tangu kuingia madarakani kwa Dk. Mwinyi, ameonekana yuko karibu mno na michezo, kiasi hata mashindano ya Kombe la Mapinduzi yameshuhudiwa yakirudisha umaarufu na msisimuko ule wa miaka nyuma na nadhani utakuwa mkubwa zaidi baadaye.

Viongozi wa soka Zanzibar wanapaswa wafanye marekebisho machache tu, ili mashindano haya yapate wadhamini wengi na kuvutia timu nyingi zaidi kuja kushiriki michuano hiyo.

Ukiangalia kwa sasa ni mijaka kadhaa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, maarufu kama CECAFA, hauna michuano ya Kombe la Afrika Mashariki na Kati (Kombe la Kagame) au mashindano ya Kombe la Chalenji kwa muda mrefu, hivyo wanaweza kuchukua nafasi hiyo wakayafanya mashindano haya yakawa makubwa zaidi.

Ninavyoona kabisa, Kombe la Mapinduzi linaweza kuchukua nafasi ya Kombe la Kagame na zikaja timu nyingi kubwa kama St.George ya Ethiopia, Al Hilal na El Merrikh ( Sudan), Gor Mahia, AFC Leopards (Kenya), KCCA, SC Villa za Uganda na nyingine nyingi.

Hapa kinachotakiwa ni kwa viongozi wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF,) kuchangamkia wadhamini.

Wakifanya hivyo nina imani baadaye itakuwa ndiyo michuano mikubwa zaidi katika CECAFA, hili linawezekana.

# ASA yaja na mikakati kuongeza usalama chakula

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WAKALA wa Taifa wa Mbegu (ASA) umeongeza hekta 5,000 za mashamba mapya ya mbegu na kufikia 17,000, zitakazoongeza uzalishaji mbegu kila mwaka na kuwa na uhakika wa usalama wa chakula.

Mtendaji Mkuu wa ASA, Dk. Sophia Kashenge, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maendeleo waliyofikia na mikakati ya mwaka ujao katika kuboresha kilimo nchini.

Dk. Sophia alisema ongezeko la uzalishaji mbegu mwaka hadi mwaka linaihakikishia nchi kuwa na uhakika wa usalama wa chakula.

Alisema wanategemea kufanya mabadiliko zaidi katika uzalishaji wa mbegu kwa sababu serikali imewekeza fedha nyingi mwaka huu na matokeo yake yatajitokeza mwakani.

Alitaja miongoni mwa mafanikio yao ni ununuzi wa matrekta mapya tisa yanayofanya idadi ya 21.

Alisema mwaka 2020 kulikuwa na matrekta manne pekee na idadi hiyo italeta mabadiliko makubwa ya uzalishaji wa mbegu.

"Tumeongeza uzalishaji wa mbegu kutoka tani 3,170 mwaka 2022 hadi 3,552 mwaka 2023 ambazo tumezizalisha. Tumefikia tani 12,000 zilizoongezeka kwa kujumlisha ushirikishwaji wa uzalishaji wa sekta binafsi na kufanya kuwa na zaidi ya asilimia 42 ya upatikanaji wa mbegu.

"Ukiangalia upatikanaji wa mbegu kwa ujumla wake tupo kwenye tani 61,000 ambapo upatikanaji wa ndani pekee ni tani 42,000 na tayari tumepunguza kuingiza mbegu kutoka nje ya nchi kwa asilimia 70 na kuzalishwa nchini," alisema.

Kiwango kikubwa cha mbegu kikizalishwa ndani ya nchi kunakuwa na imani zaidi na usalama wa chakula.

Alisema licha ya kufikia asilimia 50 ya uzalishaji mbegu, bado hawajafikia mahitaji ya tani 124,000 kwa mwaka na kukaribisha sekta binafsi zaidi ili kuongeza nguvu katika uzalishaji huo.

Dk. Sophia alisema kuna mwitikio mkubwa wa wakulima kuhitaji mbegu za wakala na mwaka 2022, walisambaza mbegu nyingi za ruzuku za alizeti na uzalishaji wa nchi umeongezeka kutoka tani 400,000 hadi kufikia milioni 1.1, mwaka huu.

Aidha, alisema ASA huzalisha mbegu za aina nyingi kulinganisha na sekta binafsi wanaozalisha mbegu za aina chache zikiwamo za mahindi na mboga.

Alisema katika msimu uliopita ASA walizalisha aina 64 za mbegu kwa kutumia maabara yao ya ndani kuhakiki ubora unaotakiwa kwa kupima tani 3,200 pamoja na sampuli mbalimbali na kupunguza gharama za kupeleka Taasisi ya Kuthibiti Ubora wa Mbegu (TOSCI) kwa ajili ya uhakiki.

Pia alisema wameongeza maghala manne katika maeneo yao na kuhifadhi tani 25,000 kwa wakati mmoja.

Kadhalika, alisema wana mashine mpya ya kufanya uchakataji na kufufua nyingine za zamani kuwa na jumla na mitambo saba ya uchakataji.

Mkurugenzi wa Uzalishaji ASA, Dk. Justine Ringo, alisema katika msimu ujao wamejipanga kuongeza uzalishaji wa mbegu kutoka zaidi ya tani 3,000 mwaka huu, hadi zaidi ya 6,000 mwaka 2024.

Alisema wamejipanga kutumia vifaa vya kisasa vya kupulizia dawa shambani na kuongeza uzalishaji pamoja na kutumia mafunzo waliyopata kuboresha mazao yao.



Naibu Waziri Mkuu, Dk. Doto Biteko, akikata utepe kufungua Zahanati ya Bungoni, Ilala jijini Dar es Salaam. Wanaoshuhudia ni pamoja na Mbunge wa Jimbo la Ilala, Musa Zungu (kushoto) na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila (kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Biteko azindua Zahanati Bungoni itakayohudumia wananchi 12,000

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, jana amezindua Zahanati ya Bungoni, Mtaa wa Mafuriko Ilala, jijini Dar es Salaam na kuwataka wananchi kutumia fursa ya huduma ya zahanati hiyo.

Zahanati hiyo itakuwa na uwezo wa kuhudumia kata nne zilizopo Wilaya ya Ilala ambazo ni Ilala, Buguruni, Sharifu Shamba na Mchikichini, huku wananchi 12,000 wakitarajiwa kuhudumiwa.

"Niwaombe viongozi wenzangu tuliopewa dhamana na Rais kuhakikisha tunawahudumia kwa vitendo wananchi na kuinua hali za wanyonge kwa kuwapatia huduma bora wanazostahili," alisisitiza Dk. Biteko.

Aliwataka wananchi wa Ilala kumpa ushirikiano mbunge wao kwa vitendo na kumpongeza kwa kazi kubwa aliyofanya ya kuleta maendeleo kwa wananchi wake na kuwataka viongozi wengine kuiga mfano wake kufanikisha ujenzi wa zahanati hiyo na kukemea wachache wanaojificha kwenye kivuli cha kuchelewesha maendeleo.

Ujenzi wa zahanati hiyo ulianza Februari, mwaka huu kwa jitihada za wananchi na baadaye serikali na umegharimu Sh. milioni 351 kwa kuhusisha ujenzi, samani, dawa na vifaa tiba.

Ujenzi huo umefadhiliwa na African Relief Agency na Taasisi ya Rahma International kutoka Kuwait na inamilikiwa kwa asilimia mia moja na serikali.

Dk. Biteko alitembelea jengo hilo linalohusisha wagonjwa wa nje (OPD), kliniki ya baba, mama na mtoto pamoja na jengo la kujifungulia na kusalimiana na kinamama waliojifungua.

Akizungungumza wakati wa hafla hiyo, Mbunge wa Jimbo la Ilala na Naibu Spika wa Bunge la Tanzania, Mussa Zungu, aliwataka watendaji kutumia vyema fursa za wafadhili wanaokuja kuwekeza kwenye sekta ya afya na kuondoa mikwamo inayochelewesha maendeleo.

Alisema Wilaya ya Ilala inapokea wageni wengi kwa siku na wananchi wenye mahitaji kwenye sekta ya afya, vituo hivyo vitasaidia kuboresha utoaji wa huduma.

Awali, akitoa taarifa ya mafanikio ya Idara ya Afya kwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Jiji, Dk. Zaituni Hamza, alisema wamefanikiwa kujenga jumla ya vituo vipya saba vya kutolea huduma na kupandisha hadhi zahanati tano kuwa vituo vya afya na kufanya jumla ya vituo vya afya kuwa 12.

Aidha, kuelekea mwaka 2025, imekuja na miradi ya kimkakati ikiwamo uanzishwaji wa Chuo cha Afya cha Kati na Sayansi Shirikishi Hospitali ya Wilaya ya Kivule na jengo la kwanza tayari limeshapauliwa, lengo ni kuunga mkono azma na dhamira ya Rais kuwaletea maendeleo karibu wananchi wake.

Dk. Zaituni alimshukuru Rais Samia kwa kuongeza bajeti kwa Wizara ya Afya hususan upatikanaji wa dawa na vifaa tiba kutoka asilimia 90.1 hadi kufikia asilimia 94 na kumwahidi kufanya kazi kwa bidii na kutoa huduma bora kwa wananchi.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Madereva pikipiki, bajaji kukiona cha 'mtemakuni'

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKUU wa Kitengo cha Usalama Barabarani mkoani Shinyanga, Wensesilaus Gumha, amesema Wilaya ya Kahama, mkoani Shinyanga, inaongoza kwa uvunjifu wa sheria za usalama barabarani hasa pikipiki na bajaji ambao hupoteza maisha na kuacha wajane na yatima.

Amesema hali hiyo imesababisha watoto kukosa mahitaji na kuanza kurandaranda mitaani.

Kamanda Gumha, aliwaonya madereva wanaokiuka sheria kwa kubeba abiria kupita kiasi watachukuliwa hatua ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa leseni na namba za usajili.

Akizungumza na waendesha pikipiki na bajaji, alisema kundi hilo limekithiri katika uvunjifu wa sheria ikiwamo kupakia abiria zaidi ya watatu.

Aliwataka kukumbuka wajibu wao ikiwa ni pamoja na kuheshimu sheria na alama za barabarani ili kuepuka ajali hasa kwa kuzidisha abiria.

Alisema kuzidisha abiria katika vyombo vya moto hasa pikipiki na bajaji husababisha ajali hasa dereva anapopata shida kidogo ya kukanyaga kitu kigumu au kupishana na gari kubwa la mizigo.

Katika kukabiliana na ajali hizo, alisema Jeshi la Polisi kupitia kikosi hicho limejipanga kuwachukulia hatua watakaobainika kwenda kinyume cha sheria.

Mwenyekiti wa Waendesha Pikipiki Mkoa wa Shinyanga (UDAPI), Idisamu Mapande, alikiri kuwapo kwa uvunjifu wa sheria za usalama barabarani kwa madereva wenzake na wakati mwingine kwa makusudi au kutokujua.

Mapande aliahidi kuendelea kuwaelimisha na kuwakumbusha madereva wenzake ikibidi kuwashauri kurudi shule kusoma ili wapate maarifa kuhusu usalama barabarani.

"Kila mwaka tumekuwa tukiongezeka na mpaka sasa pikipiki zipo 13,060, bajaji 4,000 na pikipiki za mizigo (guta) ni zaidi ya 400 na tuna vituo 45 vilivyosajiliwa kati ya hivyo, 31 ni vya pikipiki za magurudumu mawili na 14 vya bajaji," alisema.

Balozi wa Usalama Barabarani wilayani humo, Godfrey Allex, alisema huwa anashirikiana na jeshi hilo kutoa taarifa wanapoona sheria zinavunjwa na wengi wamekuwa wakichukuliwa hatua.

Mmoja wa madereva pikipiki wa kituo cha Namanga, Sayu Mashaka, alisema baadhi yao wanaponunua vyombo hivyo wanatoa baadhi ya vifaa muhimu vya kiusalama ikiwamo vioo, namba za usajili na kuandika majina yao.

Pia alisema wapo wanaobadilisha taa na kuweka zenye mwanga mkali pamoja na vimulimuli na kushauri wakikamatwa wavirejeshe kwanza kabla ya kuanza kuwajibishwa kisheria.




Baadhi ya wananchi wakivuka kwa shida kwenye lango la kuingia na kutoka eneo la Nyerere Square jana jijini Dodoma, hali hii hujitokeza msimu wa mvua. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Waomba elimu utambuzi vifungashio dawa za kulevya

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

BAADA ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) kukamata dawa za kulevya zikiwa kwenye vifungashio vyenye chapa mbalimbali za kahawa na majani ya chai, wasiwasi waibuka kwa wananchi wanaotumia bidhaa za aina hiyo.

Wameiomba DCEA kutoa elimu ya utambuzi wa vifungashio vya dawa za kulevya ili kuondoa hofu itokanayo na bidhaa kama hizo wanazonunua dukani.

Mamlaka hiyo ilitangaza kukamata dawa za kulevya zenye uzito wa kilogramu 3,182 katika msako wake jijini Dar es Salaam na Iringa.

Kwa mujibu wa Kamishna Jenerali wa Mamlaka hiyo, Aretas Lyimo, kiasi cha dawa kilichokamatwa kilikuwa kimefungashwa kwenye vifungashio vya bidhaa zenye chapa mbalimbali za kahawa na majani ya chai.

Mkazi wa Majengo Kahama, Juma Ally, akizungumza na mwandishi wa habari hizi alisema, "vifungashio vya bidhaa ya majani ya chai vipo vya aina mbalimbali, kama tutaweza kupata elimu ya kuweza kuvitambua tutakuwa mabalozi wazuri wa kuisaidia serikali kuwakamata wauzaji wa dawa hizo kupitia majani ya chai."

Ally alisema wanapata taarifa tofauti kuhusu vifungashio vya dawa hizo wakiwamo wanaotengeneza kwa kutumia biskuti.

Aidha, alisema ni wakati wa jamii kuelimishwa ili kusaidia Mamlaka ukamataji kwa kuwa wanaoharibika ni vijana.

Masanja Maduka, aliishukuru mamlaka hiyo kwa kufanya kazi nzuri na kutaka udhibiti ufike wilayani humo kwa kuwa kuna kundi la watoto ambao huvuta gundi ambayo inawaathiri kwa kiasi kikubwa na kushinda wakiwa wamesinzia.

Wananchi hao waliiomba serikali kuendelea kuwatafuta watuhumiwa hao na kuwafikisha katika vyombo vya sheria pamoja na kutia mkazo wa elimu hasa kuhusu dawa mpya ya Methamphetamine ambayo imekuwa na madhara makubwa kwa vijana.

Pia wameliomba Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kuwa makini katika bidhaa hizo zilizotajwa ili wananchi wawe na imani nazo kwa kuwa suala hilo limeleta hofu kwao.

## Kaya 119 zilizokumbwa mafuriko Moshi zakumbukwa

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

SERIKALI imetoa misaada ya vyakula, magodoro, ndoo, madumu na mablanketi kwa kaya 119 zilizoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro zilizokumbwa na mafuriko.

Akikabidhi misaada hiyo, mahindi tani 20, magodoro 150, mablanketi 300, ndoo 150, madumu 150 na mikeka 300, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Ummy Nderiananga, alisema serikali inatambua matatizo yaliyowakumba wananchi hao kutokana na mvua iliyonyesha na kusababisha mafuriko.

Hata hivyo, alitoa onyo kwa baadhi ya watu wanaotoa taarifa za uongo kupitia mitandao ya kijamii kuacha mara moja kwa kuwa wanasababisha taharuki.

"Inapotokea taarifa za maafa wapo wasemaji wake kwa mkoa ni Mkuu wa Mkoa na wilaya, sasa wapo watu wanarekodi na kusambaza taarifa za uongo kwenye mitandao na kusababisha taharuki kubwa. Niwaombe achaneni na hii tabia, tumieni mitandao vizuri," alionya.

Aliiagiza Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Moshi kukutana na Kamati ya Maafa ya wilaya pamoja na wataalamu wengine ili kuweka mikakati ya uzibuaji wa njia za Mto Nanga na Mto Manguvu ili kuzuia mafuriko katika Kijiji cha Sango, Kata ya Old Moshi.

Mbunge wa Moshi Vijijini, Prof. Patrick Ndakidemi, aliishukuru serikali kwa kuzikimbilia familia za waathirika wa mafuriko katika maeneo mbalimbali ikiwamo Wilaya ya Hanang, mkoani Manyara.

Prof. Ndakidemi, alisema katika maafa hayo yaliyosababishwa na mvua, watu watano walifariki dunia pamoja na mashamba na vitu mbalimbali vikiwamo vyakula kusombwa na mafuriko.

"Msaada uliotolewa na serikali utasaidia kuzifariji familia zilizokumbwa na mafuriko na waathirika, hatua hii ni kuonyesha namna ambavyo serikali inawathamini," alisema Prof. Ndakidemi.

Mkuu wa Wilaya ya Hai, Amir Mkalipa, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Moshi, aliutaka uongozi wa halmashauri kugawa vitu hivyo kulingana na maelekezo ya serikali na yeyote atakayekiuka atamchukulia hatua.

Baadhi ya waathirika wa mafuriko waliishukuru serikali kwa kuwajali wananchi wakati wote wanapokumbwa na matatizo hatua ambayo huwapa faraja na kusaidia kurejesha hali.



## Wazazi wakumbushwa kupeleka shule watoto waliofaulu

**Na Renatha Msungu,** KONDOA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, Hassan Mtamba, amewaagiza wazazi wilayani hapa kuhakikisha watoto wote waliofaulu wanajiunga na kidato cha kwanza mwakani kabla ya hatua za kisheria hazijachukuliwa dhidi ya wale watakaokaidi agizo hilo.

Mtamba, alisema hayo juzi wakati wa kikao cha Kamati ya Ushauri cha Wilaya ya Kondoa (DCC) kilichoketi kwa ajili ya kujadili masuala mbalimbali ya kimaendeleo ya Wilaya ya Kondoa kwa kipindi cha Juni hadi Desemba, 2023.

Alisema, jumla ya wanafunzi 1,794 wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2024 na kila mzazi ahakikishe mtoto wake anaenda shule aliyopangiwa kabla ya hatua za kisheria hazijachukuliwa dhidi ya wazazi hao.

"Hatutarajii kuona mzazi anasema hajajiandaa kwani kwa kipindi chote hiki tunajua mtoto anapaswa kuwa shule tufanye maandalizi mapema ili Januari wawe shule wote na mahitaji ya shule na kwa ambao watoto hawataenda shule wazazi mtawajibishwa," alisema.

Katibu Tawala Wilaya ya Kondoa, Christina Kalekezi, aliwataka wazazi kutoa kipaumbele kwenye elimu ya watoto wao.

Akizungumza katika kikao hicho, Kalekezi amezipongeza halmashauri za wilaya ya Kondoa kwa kuinua kiwango cha ufaulu mwaka hadi mwaka jambo ambalo linatakiwa kuungwa mkono na wazazi wa wilaya hiyo.

"Tukiwa na utayari watoto wetu watafanya vizuri, lakini hapo wazazi tukiamua na tukikubaliana jambo tunapaswa kufanya kwa pamoja hasa kuhakikisha kuwa watoto wetu wanapata elimu bora na hakuna atakayekuja kulalamika," alisema.

Aidha, serikali imewekeza katika elimu kwa kuhakikisha miundombinu inajengwa na kuhakikisha walimu wanapatikana hivyo ni jukumu la viongozi wa ngazi zote ikiwamo vijiji, mitaa na kata kuwa jambo hilo wanalipeleka kwa pamoja na wakiamua wanaweza kuinua elimu.

"Tuige mfano kwa wenzetu wa mkoa wa Kilimanjaro wao wanajenga shule wenyewe wanaomba walimu tu kwa serikali na wanafanya hayo kwa kuwa wana utayari ambao nasi tukiwa nao tunaweza kuwafikia hivyo tukaamue kuwakomboa watoto wetu bila kujali si wako kwa kuwa ukimsaidia leo huyu kesho atakusaidia pia," alisema.

# TGNP yapendekeza masuala ya kijinsia kuwekewa bajeti

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MTANDAO wa Jinsia Tanzania (TGNP) umeishauri serikali kujumuisha masuala ya kijinsia katika mipango ya maendeleo, sera na bajeti ili makundi yote nchini yafikiwe kikamilifu.

Mtafiti na mchambuzi wa masuala ya jinsia kutoka TGNP, Wilfred Kulwa, alibainisha hayo juzi jijini hapa kwenye mafunzo yaliyoandaliwa na taasisi hiyo kwa maofisa kutoka wizara 13 za kisekta nchini.

Alisema mafunzo hayo lengo lake ni kuwajengea uwezo maofisa hao kujumuisha masuala ya kijinsi kwenye mipango yao na bajeti katika sekta zao.

Alisema, pamoja na mambo mengine wizara hizo za kisekta zinapaswa kuendelea kupanga mipango ya maendeleo kwa kuzingatia utafiti kuwamo Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS).

"Mafunzo haya kwa maofisa hawa wa wizara hizi za kisekta yatawasaidia kuongeza uwezo wa kujumuisha masuala ya jinsia kwenye mipango yao pamoja na bajeti zao pia yatasaidia walengwa wanaohusika katika sera na kujijengea uwezo kwenye masuala ya jinsia kwa ujumla," alisema Kulwa.

Pia alisema changamoto hivi sasa ni wahusika katika wizara kushindwa kutumia utafiti na uchambuzi ambao umefanywa ili kujumuisha masuala ya jinsia katika sekta mbalimbali nchini.

Naye Mraghbishi na Mtafiti Mwandamizi wa masuala ya kijinsia nchini, Dk. Geofrey Chambua, alisema ili masuala ya kijinsia yaeleweke katika jamii ni vyema yasilenge kundi la wanawake pekee.

Dk. Chambua, alisema viongozi katika wizara wanapaswa kuondokana na mawazo mgando kuwa suala la jinsi ni la mwanamke pekee.

Alisema ipo haja kwa wakuu wa taasisi na wizara kuendelea kutenga rasilimali fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya majengo kuwa rafiki kwa makundi yote.

Alisema siyo jambo zuri kwa wakati huu kukuta jengo la serikali sio rafiki kwa watu wenye ulemavu au halina chumba kwa ajili ya kunyonyeshea au vyoo kwa watu wenye ulemavu.

Vile vile, ipo haja ya serikali kutenga fedha kwa ajili ya mafunzo ya kuwajengea uwezo wataalamu wake ambao wamekuwa wakihusika na masuala ya mipango na bajeti ili ziwe na mrengo wa kijinsia.

"Wataalamu wengi wamekuwa wakifanya mipango yao wakiwa ofisini hawatumii takwimu za ofisi ya Taifa ya Takwimu kupanga mipango itakayo jumuisha makundi yote kwa kuzingatia takwimu za makundi hayo," alisema Dk. Chambua.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri (katikati), akisoma nyaraka za wakazi wa Ntyuka jijini humo, wanaotakiwa kupisha maeneo kwa ajili ya ujenzi wa barabara jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Ahimiza miradi elimu ikamilike kuondoa usumbufu

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, amezitaka halmashauri za wilaya mkoani hapa kukamilisha miradi ya maendeleo kwa wakati ikiwamo ya elimu ili wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari waweze kuanza masomo ifikapo Januari mwakani.

Alisema hayo jana wakati akizungumza na wazazi, walezi na viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi katika Shule ya Msingi Kintandaa baada ya kukagua miradi ya maendeleo kwenye kijiji cha Irisya, Msimii, Kipunda na Kintandaa ikiwa ni mwendelezo wa ziara ya kusikiliza na kutatua kero za wananchi katika kila kijiji mkoani humo.

Serukamba alilazimika kutoa maelekezo hayo baada ya kujionea ujenzi wa vyumba vya madarasa ya shule hiyo na ambayo yapo kwenye hatua mbalimbali za ujenzi.

"Mkurugenzi, lijulishe baraza lako la madiwani juu ya ujenzi wa vyumba vya madarasa... hakikisha mnakamilisha mapema kabla ya Desemba 31, mwaka huu ili ifikapo Januari mwakani, wanafunzi waweze kuyatumia katika masomo yao," alisema.

Aidha, katika kituo cha afya Irisya, Serukamba, alimtaka Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Ikungi, Alli Mwanga, kulielekeza Baraza la Madiwani liidhinishe fedha za kukamilisha miradi ya zahanati na vituo vya afya ili wananchi waanze kunufaika na matunda ya serikali yao ya awamu ya sita.

"Kwenye miradi hii yote, hakikisheni mnaisimamia vizuri na kuifuatilia mwanzo hadi mwisho ili iweze kuendana na kasi, ubora, thamani ya fedha na kiwango kinachostahili, kwa lengo la kuleta tija kwa jamii yetu tunayoitumikia," alisisitiza.

Aliipogeza serikali kwa kuwaletea wananchi maendeleo kupitia miradi ya afya elimu maji na miundombinu ya barabara.

"Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, sisi wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, pamoja na mambo mengi ya maendeleo yanayoendelea hivi sasa, tunamshuru sana Rais wetu, Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kutupatia fedha za kutosha kwa ajili ya miradi mbalimbali inayotekelezwa," alisema.

Pia aliwaomba wananchi waendelee kumuunga mkono Rais, kutokana na kazi kubwa ya maendeleo anayoifanya ya kuwajali Watanzania na bila kubagua kwa misingi ya dini na kabila lake la asili.

Ziara hiyo ni mahusus kutembelea vijiji vyote 441 vya Mkoa wa Singida, huku katika awamu ya kwanza akiwa amekamilisha kukutana na wananchi wa vijiji zaidi ya 61, kwa ajili ya kusikiliza na kutatua kero mbalimbali zinazoikabili jamii.



## HABARI ZANZIBAR

# Malaria tishio Z'bar, yaua watu 36 miezi miwili

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KASI ya wagonjwa wa malaria Zanzibar inazidi kuongezeka huku watu 36 wakifariki toka mwezi Novemba hadi Desemba, mwaka huu.

Akizungumza jana na Nipashe ofisini kwake Mnazi Mmoja, Waziri wa Afya Nassor Ahmed Mazrui, alisema kasi ya ugonjwa huo inatokana na mwingiliano wa safari kati ya Zanzibar na Tanzania Bara pamoja na kuongezeka kwa mazalia ya mbu.

Alisema kwa mwaka 2023 Zanzibar imepata wagonjwa wa malaria 12,000 na mwaka jana ilikuwa na wagonjwa 4,000.

"Hali si nzuri wagonjwa wa malaria ni wengi na serikali inaendelea kupambana kukabiliana nayo ikiwamo kupiga dawa ya malaria mitaani na majumbani," alisema waziri.

Kadhalika, hatua hiyo ya upigaji wa dawa imesaidia kuondoa mazalia ya mbu na kuwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari ya kupambana na ugonjwa huo ambao unaua.

Alisema miongoni mwa hatua zinazostahili kuchukuliwa ni kutumia vyandarau wakati wa kulala, kupiga dawa na kufanya usafi wa kudhibiti mazalia ya mbu.

"Malaria ipo na inaua wagonjwa wengi katika hospitali na vituo vya afya, niwaombe wananchi wanapohisi dalili ya kuumwa homa wasikae nyumbani na badala yake kukimbilia kituo cha afya kwa ajili ya kupata matibabu mapema kabla ya athari ya ugonjwa haujawa mkubwa," alisema.

Alisema mbu wa malaria wana kasi kubwa ya kushambulia mwili wa binadamu na baadhi ya wagonjwa waliofariki iliwapiga hadi katika ubongo, ini na figo.

Alisema kinga ya mwili imeshuka kwa baadhi ya wananchi na wanaposhambuliwa na mbu wa malaria huathirika zaidi na ugonjwa huo.

Alisema waandishi wa habari wana nafasi kubwa ya kuelimisha jamii ya kujikinga na kudhibiti magonjwa mbalimbali ya kuambukiza na yasioambukiza ili kudhibiti madhara ambayo yanaweza kuepukika.

Nipashe ilitembelea baadhi ya vituo vya afya na Hospitali Mjini Unguja na kukuta msururu mkubwa wa wagonjwa waliogundulika kuwa na malaria wakiendelea kupatiwa matibabu.

Mmoja wa wahudumu katika vituo hivyo ambaye hakutaka kutajwa jina lake alisema kwa siku hupokea wastani wa wagonjwa 15 wa malaria.

Alisema wengi wa wagonjwa wa malaria ni vijana wa kiume na anahisi mbu hao wapo mitaani zaidi sio majumbani.

"Wengi wa wagonjwa wa malaria tunaowapata ni wanaume tena ni vijana nadhani malaria zaidi ipo mitaani maana vijana wengi hupenda kukaa maskani na vijiweni maana wanawake sio wengi tuliowapata kituoni hapa wenye malaria," alisema.

Mmoja ya wagonjwa wa malaria Fatma Juma (sio jina halisi), mkazi wa Kwahani Mjini Unguja, alisema yeye na watoto wake wawili wamepata ugonjwa wa malaria na kupata matibabu mazuri hospitalini.

"Kwanza nilianza mimi kupata homa kali nikiwa nimo katika boti natoka Dar es Salam nakuja Zanzibar na nilipoenda hospitali nikagundulika kuwa na malaria kisha watoto wangu wawili, mmoja ana umri wa miaka sita na mwingine miezi tisa wakapata homa na nilipoenda hospitali wakagundulika kuwa na malaria na kwa sasa tunaendelea na dozi," alisema.

Aidha, aliipongeza serikali kwa kuboresha huduma za afya na matibabu yote aliyoyapata yeye na mtoto wake ikiwamo dawa na vipimo alivyopatiwa bure.




Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Abeida Rashid Abdallah (kushoto), akimkabidhi cheti cha shukrani Mratibu wa Mafunzo ya kuwajengea uwezo kikundi cha Banaty, Raya Hamad Mchele, Michenzani Unguja juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yakiri mfumo malipo kidijitali umedhibiti upotevu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Dk. Sada Mkuya Salum, amesema mfumo wa malipo kwa njia ya kidijitali umesaidia kudhibiti mianya ya upotevu wa fedha.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa wizara hiyo.

Alisema uchumi wa nchi umekua kutokana na mikakati imara ya kiuchumi iliowekwa na serikali.

Alisema uchumi huo umekua kwa asilimia sita jambo ambalo ni tofauti na mataifa mengine duniani.

Pia, pamoja na changamoto nyingi za sayansi na teknolojia zilizopo duniani, wamefanikiwa kukuza uchumi kwa kiasi kikubwa.

"Inawezekana mifumo imara iliyopo hivi sasa ya kuhesabu pengine imechochea kuimarika kwa uchumi wetu Zanzibar," alisema Waziri Mkuya.

Alisema kwa sasa wanakwenda kimataifa zaidi na inatarajiwa mwaka 2024 uchumi kukua hadi kufikia asilimia 6.5.

Aidha, sera ya serikali ya ukusanyaji wa kodi imejikita katika uchumi wa buluu na ndani ya sera hiyo, wizara imeweka miongozo kupitia kwenye malengo ya muda mrefu ya miaka 50 na malengo ya muda wa kati 2021 hadi 2026.

Alisema Zanzibar inategemea uzalishaji kutoka nchi za nje, lakini kwa mipango thabiti ya uchumi iliyopangwa na serikali, itasaidia kukuza uzalishaji wa ndani na watahakikisha wanasimamia suala hilo na kupunguza hali ya utegemezi wa kutegemea chakula kutoka nje ya nchi.

Mkuya alisema Zanzibar ni nchi ya kwanza kwa nchi za Afrika kufanikiwa kuwalipa pensheni wazee kuanzia miaka 70 kwa kiwango cha Sh. 50,000 jambo ambalo ni mwelekeo nzuri katika ustawi wa jamii.

# Dk. Shein asema sekta za maendeleo zimeimarishwa visiwani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS mstaafu, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema serikali inaendelea kuimarisha sekta za maendeleo ya wananchi ili kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kuwaondolea wananchi changamoto za maisha.

Akizungumza jana katika ufunguzi wa Hospitali ya Mbuzini, Wilaya ya Magharibi "A" Unguja ikiwa ni shamrashamra za maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar, alisema sekta ya afya imeimarishwa kwa kiasi kikubwa ili kutoa huduma bora na rafiki kwa wananchi.

Alisema serikali imetumia fedha nyingi kuimarisha huduma za afya ikiwamo kujenga hospitali za wilaya na mkoa, kuajiri madaktari wapya kwa lengo la kuwafikishia huduma bora na rahisi wananchi na kuondoa mrundikano wa wagonjwa katika Hospitali ya Rufani Mnazi Mmoja.

Alisema ufunguzi wa hospital hiyo ni miongoni mwa ahadi za Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliyoitoa wakati wa kampeni za uchaguzi wa mwaka 2020.

Aidha, aliwataka wananchi kuyaenzi na kuyalinda matunda ya Mapinduzi ili azma ya Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Hayati Mzee Abeid Karume kuwapatiaa matibabu bora wananchi iweze kufikiwa.

Vile vile, serikali imeyaenzi na kuyalinda matunda hayo kwa kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa hospitali za wilaya na mkoa, barabara zenye kiwango cha lami, majengo ya shule za ghorofa pamoja na masoko ya kisasa.

Akitoa taarifa ya kitaalamu kuhusu ujenzi wa hospitali hiyo, Kaimu Katibu Mkuu na Mkurugenzi Mkuu Wizara ya Afya, Dk. Amour Seleiman, alisema jumla ya Sh. bilioni 8.5 zimetumika katika ujenzi huo.

Alisema hospitali hiyo inatoa huduma kwa wananchi ikiwamo ya mama na mtoto, uchunguzi wa maradhi mbali mbali na huduma ya dharura inapohitajika kwa haraka.

Hospitali hiyo ina uwezo wa kulaza wagonjwa 100 na hadi sasa imeshaanza kuhudumia wananchi zaidi ya laki tatu.

Imejengwa na Kampuni ya CRJE kutoka China iliyogharimu Sh. bilioni 8.5 katika ujenzi ikiwa ni shamrashamra za kuelekea maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar.



SHUSHO
UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI DESEMBA 30, 2023




# BILA MISSO MISONDO hujamaliza 2023

MWAKA 2023 unamalizika ukiandamana na 'vaibu' la nguvu kutoka kwa kijana mdogo anayefahamika kama Misso Misondo, ambaye utaalamu wake wa kuchezesha muziki umesababisha watu kila rika wanatikisa vichwa bila kupenda.

Huyo ndiye Misso Misondo kijana wa miaka 28 kutoka Masasi mkoani Mtwara, ambaye kwa sasa amekuwa habari ya mjini kwa uburudishaji kuanzia vituo vya redio hadi katika mitandao ya kijamii.

Pengine hakutarajia jina lake lingeweza kumaliza mwaka likiwa anga za juu na kusababisha watu kushindwa kupata usingizi kutokana na aina ya muziki wake wenye ladha adimu iliyochanganywa na ngoma za makabila mbalimbali.

Katika miezi michache hakuna aliyejaribu kulizima jina lake, na hata wale waliotaka kubadilisha upepo kwa kutambulisha wasanii wao, wamejikuta wakikumbwa na dhoruba kali la Misso Missondo na kujikuta wanacheza midundo yake bila kupenda.

Upepo wa Misso Misondo umemkumba kila mtu, ukiwa ndani ya daladala, bodaboda, bajaji na hata magari ya watu wazito utasikia 'We Misso Misondo umepigaje hapo?

Hakika ni jambo la kumpongeza kijana huyu kutokana na ubunifu wake wa kuingiza muziki wa Singeli na ngoma za makabila mbalimbali, huku ikinogeshwa na wachezaji wake wazee wa masuti na kumfanya kila mtu kuwehuka.

Licha ya baadhi ya watu kujitokeza kumsaidia kusonga mbele, lakini serikali inatakiwa kumwona kwa macho makali ikiwa pamoja na kumwezesha kitaalamu ili kazi zake ziwe bora na zifike mbali.

BASI SAWA

## Jitubaya afunga mwaka na 'Tutavuka Border'



RAPA anayekuja kwa kasi, Jitubaya Flow, ametamba kuwa mwaka 2023 umekuwa wa mafanikio kwake baada ya ngoma zake kuwa miongoni mwa zilizotamba.

Akizungumza na BT, wakati akitambulisha video ya ngoma yake mpya inayoitwa 'Tutavuka Border' amesema ndani ya mwaka huu amefanya vizuri kisanii na wimbo huo ambao umebeba ujumbe wa vijana kupambana kwenye sekta utakuwa kama wa kufungia kazi.

"Huu wimbo ni meseji kwa mataifa yote hasa vijana wapambanaji jinsi ya kupambana tuweze kutoka chini hadi kiwango cha juu na ndio utakuwa wa kufungia mwaka kwa upande wangu," amesema.

## Shusho kuitikisa Kenya mkesha Mwaka Mpya



MWIMBAJI wa muziki wa Injili, Christina Shusho, atakaribisha mwaka mpya 2014 akiwa nchini Kenya baada ya kualikwa katika tamasha litakalofanyika jijini Nairobi.

Shusho atatumbuiza katika tamasha hilo litakalofanyika usiku wa mkesha na kuwakutanisha wasanii maarufu wa nyimbo za injili kutoka nchini humo.

Amesema anafurahia kumaliza mwaka 2023 na kuanza mwaka mpya akiwa nchini Kenya na hiyo ni zawadi tosha kwa mashabiki wake wengi ambao kila mara wanataka kuwa naye karibu.



## DIAMOND HAKUNA KAMA YEYE 2023

MWANAMUZIKI nyota wa Bongo Fleva, Diamond Platnumz, amemaliza mwaka 2023 kwa kuonyesha ukubwa wake mbele ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi kwa kufanya shoo ya kibabe.

Diamond ambaye alikuwa mwanamuziki mwalikwa katika ufunguzi wa Uwanja wa Amani, ameonyesha yeye ni kinara wa ubunifu na uburudishaji hasa katika eneo lenye mashabiki wengi.

Hata katika kurasa zake za kijamii, mwanamuziki huo ameonekana akijigamba kwamba amemaliza 2023 katika hali ya matumaini baada ya kufanya vizuri katika shoo yake hiyo.

Kiujumla Diamond licha ya kuonekana kama anasuasua kimuziki, lakini kile alichokionyesha mbele ya viongozi wakuu na wananchi waliohudhuria katika ugunduzi huo ni tosha kueleza hakuna tena kama yeye katika suala la kulitawala jukwaa.

## FILAMU

## Elis: Damu haipotei

**Na Adam Fungamwango**

NI stori ya kusikitisha kwa kweli. Waswahili wana msemo unaosema damu haipotei. Hili ndilo tunaweza kuthibitisha kwenye filamu hii ya 'Elis.'

Imechezwa na wasanii kina Lawrence Munga, Simon Mwapagata, Stephen Mtambo, Angel Nassir, Shamsa Ford, Tibera Katesingwa na wengineo.

Jijini Kigoma, Simon, mmoja wa wakimbizi kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, anaondoka kwenye kambi na kwenda kujenga maeneo mengine akiwa na familia yake.

Mtoto wake Elis, anapata kazi ya kumsaidia mama mmoja mgahawani. Hata hivyo baada ya miezi kadhaa anapata ujauzito unaomfanya asiendelee kufanya kazi pale.

Baba yake naye anamtimua nyumbani, hivyo anaamua kupanda treni kuelekea Morogoro kumsaka aliyempa ujauzito, ambaye wakati wa mahusiano alimwambia anaishi huko na jina lake ni James. Alipofika huko hakumkuta James. Akaangulia kwenye mikono ya dada mmoja msamaria mwema ambaye ambaye alimshauri kufanya biashara.

Kwa bahati mbaya wakati anajifungua, Elis alifariki. Akakiacha kichanga, ambacho kilichukuliwa na kulelewa na Happyness, rafiki yake Elis aliyempokea.

Naye anafariki kutokana na maradhi ya ukimwi. Mtoto anaangukia mikononi mwa dada wa Happyness ambaye aliamua kukichukua kichanga na kukilea jijini Dar es Salaam.

Hata hivyo dunia haina siri, kijana Harun anakuja kugundua kuwa anayemlea si mama yake mzazi.

Anasimuliwa kisa kizima kilichotokea, naye anaamua kuelekea jijini Kigoma kusaka ndugu zake.

Anayemkuta huko ni dada wa mama yake Djodjo, lakini kwa bahati nzuri anapata picha kamili ya mama yake alipotokea na kukutana na wale wote ambao waliishi na mama yake Elis, hususan alikuwa anafanya nao kazi mgahawani.

Anaridhika na kurejea jijini Dar es Salaam. Anaanza kutafuta kazi baada ya kumaliza chuo.

Meneja mwajiri mmoja baada ya kuangalia vyeti vya kijana yule na kumuuliza maswali kadhaa anagundua kuwa ni mtoto wake.

Anamwambia kuwa yeye ndiye aliyempa ujauzito Elis ambaye ni mama yake, lakini hakuweza kukaa Kigoma kwa sababu za kikazi.

Baba anamwomba msamaha kijana wake na kumwambia yaishe, kwani amefika mahali salama kwa mzazi wake halisi.







## Amos Acrobatics aomba kura

MSANII wa sanaa ya viungo nchini, Amos Acrobatics ameteuliwa kuwa miongoni mwa watu walioteuliwa kuwania tuzo zitakazotolewa mapema mwakani.

Amos ambaye ni maarufu kwa kuburudisha kwa kutumia viungo vya mwili, atawania katika kipengele cha mwanasarakasi bora katika tuzo zitakazotolewa na Chama cha Mazoezi ya Viungo Tanzania mwaka unaokua.

Amewataka Watanzania kumpigia kura ili kupata tuzo hiyo akiamini itakuwa njia pekee ya kumfanya ajivunie sanaa yake.

Upigaji kura unafanyika kwa kutumia Baba App ambayo huko utapiga kura baada ya kufuata maelekezo.

## PESA INAVUNJA BONDE NA MILIMA

**Na Adam Fungamwango**

DUNIA ilipofika sasa kila kitu ni pesa. Huwezi kufanya lolote bila pesa. Mama mjamzito tu mpaka ajifungue salama na kurejea nyumbani, inabidi pesa zitumike.

Kukitunza kichanga mpaka kikue, kupeleka mtoto shule, matibabu yaani kila kitu ni pesa.

Kwa wale ambao wanaishi mijini ndiyo kabisa, kuanzia vocha, bando, kujaza gesi kwenye jiko, kulipia king'amuzi, umeme, taka na ulinzi, vyote hivi vinahitaji pesa.

Hata huko zamani ambapo hakukuwa na matumizi makubwa kama haya ya sasa, wazee walishaanza kutabiri kuwa mbele ya safari pesa itatawala dunia.

Ndiyo maana wakaja na msemo kuwa pesa sabuni ya roho. Pesa penye udhia penyeza rupia.

Hata mapenzi, yanastawi pale ambapo kuna pesa, vinginevyo hata kama yatakuwapo lakini yatanyauka tu.

Na wanamuziki wa zamani walitunga nyimbo mbalimbali kuhusu pesa. Hebu tuone mitazamo yao na jinsi walichokisema.

### Pesa Zanisumbua - Dudumizi

Wimbo huu ulirekodiwa katikati ya miaka ya 1980 na bendi ya Bima Lee. Ulikuwa ni utunzi wa Jerry Nashon 'Dudumizi', unaitwa 'Pesa Zanisumbua.'

Mtunzi katika wimbo huu anamwambia mpenzi wake kuwa asione kimya mpaka sasa wanachelewa kufunga ndoa, ni kwa sababu pesa zinamsumbua.

Anamkumbusha mpenzi wake kuwa anampenda sana na alihitaji kuharakisha hilo, lakini bado yupo kwenye harakati ya kusaka pesa na mambo yakiwa mazuri, wataoana.

### Pesa Sabuni ya Roho-Marijani

Miaka hiyo hiyo ya katikati ya 1980, Marijani Rajab, akiwa na Dar International alitunga na kurekodi kibao kiitwacho 'Pesa sabuni ya Roho.'

Maudhui ya wimbo huu ni mtu anayelalamika kuchukuliwa mpenzi wake Helena na mtu mwenye pesa.

Alikuwa na mpenzi wake huyo na kuahidiana kuoana, lakini akatokea kibopa na kumrubuni na kumvika heleni na bangili za dhahabu, akampindua.

Jamaa anakiri kuwa kweli mwenye pesa siyo mwenzio na yeye sasa anasema anaanza kuzitafuta pesa kwa nguvu na kwa bidii kihalali ili naye awe na pesa.

### Pesa - Dk. Remmy Ongalla

Mwanzoni mwa miaka ya 1980, Dk. Remmy Ongalla alifyatua kibao cha 'Pesa.'

Lengo ni lile lile, kuonyesha pesa ilivyokuwa na nguvu kwenye jamii.

Anakwambia, popote unapokwenda bila pesa hakuna mafanikio, ukiwa na pesa popote unapotaka utafika.

Halafu mwishoni anawashauri watu kuwa unapotafuta pesa usione aibu na usichague kazi.

### Mtu Pesa-Banza Stone

"Atapata kila kitu isipokuwa amani, atakwenda kila mahali isipokuwa peponi, atajulikana kila mahali, isipokuwa mbinguni, atarithi kila kitu ila uzima wa milele."

Ni maneno yanayopatikana kwenye wimbo wa 'Mtu pesa', utunzi wake marehemu, Banza Stone akiwa na bendi ya African Stars 'Twanga Pepeta', uliorekodiwa mwanzoni 2011.

Maneno yenyewe yanajitosheleza, sina haja ya kuongea, bali unajieleza wenyewe.

### Pesa Kama Maua-Lovy Longomba

Mwanzoni mwa miaka ya 1980, mwanamuziki Lovy Longomba alipotoka African Sound Orchestra, 'Afriso Ngoma' alitengeneza bendi yake akaiita Super Lovy.

Moja ya wimbo aliourekodi ni 'Pesa Kama Maua.'

Anaiuliza pesa imeumbwa na nani? Kwa nini inasumbua watu? Katika mazuri ipo. mabaya pia upo. Kukupata wewe shida, ukipatikana matatizo, tukuelewe vipi?



# Ireti kumbe ana aibu

MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Ireti Doyle, amefichua kwamba kabla ya kuingia katika tasnia hiyo alikuwa na aibu kuwaambia watu kwamba anataka kuigiza.

Ireti amesema wakati akiwa na kazi yake ya uuguzi alitamani sana kcheza filamu, lakini alitawaliwa na aibu kiasi ambacho hakuweza kusema hitaji lake kwa watu wengine.

"Nilikuwa na aibu, sikuweza kusema kwa sauti nini nahitaji. Sijui hata kwa nini lakini sasa ninafikiri nini kingetokea, nilichojua ni kwamba nilitaka tu kuchukua hatua." Alisema.



## Portable hataki mchezo

MWANAMUZIKI mwenye utata kutoka Nigeria, Habeeb Okikiola maarufu Portable', ameshinda katika pambano la masumbwi dhidi ya mwigizaji Charles Okocha.

Katika shindano la ndondi lilowahusisha mastaa nchini humo lilofanyika Desemba 27, kwenye ufukwe wa Landmark jijini Lagos Portable aliwakilisha bukta ya buluu na huku Okocha amevaa nyekundu.


Katika video zilizosambaa kwenye mitandao ya kijamii, Okocha alionekana akijaribu kukwepa ngumi za Portable bila mafanikio na kumfanya ayumbe na kisha kuanguka chini.


## Card B sema ukweli

RAPA maarufu kutoka Marekani, Cardi B amekanusha uvumi unaosambaa kwamba amerudiana na mume wake wa zamani Offset, baada ya wawili hao kuonekana wakisherehekea sikukuu ya Krismasi wakiwa pamoja na watoto wao.

Cardi B ameandika kupitia ukurasa wake wa X kwamba yeye na Offset hawajarudiana na wanachokifanya ni kuwa pamoja na watoto wao kufurahia sikukuu na sio vingine.

Ingawa sababu ya kuachana kwao imekuwa siri, Cardi ameeleza kwamba mume wake huyo wa zamani alikuwa akimsaliti wakati wakiwa pamoja.





## Angela umelianzisha mwenyewe

MWIGIZAJI wa Nollywood, Angela Okorie, ameibua mjadala mitandaoni baada ya msanii huyo kutumia kinywaji cha champagne kunawia mikono yake kama ishara ya kuwa na mafanikio katika maisha yake.

Angela aliweka video mtandaoni akiwa kwenye klabu akisafisha mikono yake na 'champagne' yenye gharama kubwa, huku akisema yeye ni miongoni mwa watu waliofanikiwa zaidi.

Hakuishia hapo, msanii huyo aliijigamba kuwa katika hali ngumu ya uchumi, lakini hawezi kunawa mikono kwa maji ya kawaida na badala yake alikuwa akitumia kinywaji hicho kinachoitwa Dom Ps.

## Arigga mzazi akosei

RAPA maarufu wa Nigeria, Erigga amemkosoa baba yake kuwa anataka kunufaika na utajiri wake ingawa alimtelekeza akiwa mdogo.

Erigga amefichua kuwa mzazi wake huyo alikataa kumlea wakati akiwa na umri wa miaka minane na kwamba ilimbidi ajitafutie riziki yeye mwenyewe.

"Unapoona wazazi wanaanza kuhisi kuwa wana haki, haileti maana kwa sababu ulikuwa na miaka mingi mbele yangu lakini hukutimiza wajibu wako, nilihusika katika mambo mengi ambayo siwezi hata kusema lakini huwa najiuliza tu kama ningepigwa risasi au kukamatwa angekuja kutaka utajiri wangu? Alihoji.





## ADC yajiweka sawa uchaguzi wa serikali za mitaa

**Na Oscar Assenga,** TANGA

CHAMA cha Alliance for Democratic Change (ADC), kimeanza kujiweka sawa kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika mwaka ujao, baada ya kutangaza kufanyika kwa uchaguzi wa ndani wa chama hicho mwaka 2024.

Jana, Katibu Mkuu wa ADC Taifa, Doyo Hassan, alisema kwa mujibu wa katiba ya chama hicho, toleo la tatu la mwaka 2019, uchaguzi wa viongozi ndani ya chama hufanyika kila baada ya miaka mitano.

Alisema tamko hilo limetajwa katika katiba yao, kwenye sura ya nane, ibara ya 53 (i), ikionyesha ukomo wa uongozi ni miaka mitano.

Aidha, alisema mwaka 2024, viongozi walioko madarakani wanatimiza miaka mitano tangu kufanyika uchaguzi na mkutano mkuu husika kwa madhumuni ya kuchagua viongozi ambao wako madarakani hadi muda huu.

"Kwa kuzingatia utekelezaji wa miongozo kutoka katika katiba yetu, Ofisi ya ADC makao makuu, inatoa ratiba ya uchaguzi wa ndani ya chama hicho kwa mwaka 2024," alisema.

Alisema uchaguzi huo ngazi ya tawi utaanza Januari mosi na utafikia ukomo wake Januari 31, mwaka ujao; wakati ule wa kata na wa majimbo, utafanyika kati ya Februari mosi hadi 29.

Uchaguzi ngazi ya wilaya na kanda, utaanza Machi mosi na utafikia ukomo Machi 31, mwaka ujao.

Uchaguzi mkuu wa chama hicho utafanyika Mei mwakani ili kupata safu mpya za uongozi.

**Alisema tamko hilo limetajwa katika katiba yao, kwenye sura ya nane, ibara ya 53 (i), ikionyesha ukomo wa uongozi ni miaka mitano.**

# Vivutio utalii Kilimanjaro kutumika kuongeza mapato

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Angelah Kairuki, ameagiza wahifadhi wa Idara ya Malikale inayohusisha pia shughuli za urithi wa utamaduni, kuviorodhesha vivutio vyote vya utalii vilivyoko katika Mkoa wa Kilimanjaro ili vitoe mchango wa mapato yanayotokana na sekta hiyo.

Kwa sasa sekta ndogo ya makumbusho na maeneo ya urithi yako hoi kutokana na udhaifu katika kuyatambua yanayoweza kuliingizia taifa fedha nyingi za kigeni.

Kairuki, aliagiza juzi kuorodheshwa kwa vivutio hivyo, akiwa katika mji wa Moshi, mkoani Kilimanjaro, alipokwenda kufunga Tamasha la Taasisi ya Utamaduni wa Kilimanjaro (KCF).

Vivutio vilivyoko katika Mkoa wa Kilimanjaro ambavyo havijaorodheshwa chini ya Idara ya Malikale ni pamoja na mapango ya asili ya Chagga Curve yaliyoko Marangu na Nubi Curve yaliyoko Kibosho Kirima na Maporomoko ya Maji Marangu, Wilaya ya Moshi.

Vingine ni Chemichemi ya Majimoto iliyoko Wilaya ya Hai, Ziwa Chala lililoko Wilaya ya Rombo na Mbokomu ambako kuna mti mkubwa na mrefu kuliko yote barani Afrika.

Katika tamasha hilo, Waziri Kairuki, alizindua mpango mahususi unaohusu matumizi ya nyumba za wenyeji zilizo na nafasi katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Kilimanjaro kwa ajili ya kukabiliana na idadi kubwa ya wageni wanaofurika kutoka nje ya nchi na nje ya mkoa huo.

Mpango huo ambao umebuniwa na Taasisi ya Utamaduni wa Kilimanjaro (KCF), unaonyesha kuwa wenyeji kunufaika na mpango huo wa 'Home Stay' kwa kupata mgawo wa asilimia 60, watoa huduma (Housekeeping Service Providers) watapata asilimia 25 na asilimia 15 itakuwa ni gharama za uendeshaji za KCF.

Awali, Mwenyekiti wa KCF, Ansi Mmasi, alisema programu hiyo inatoa fursa kwa wananchi wa Kilimanjaro, kujisajili na kuruhusu nyumba zao zitumike kwa malazi ya wageni watakaofika kwa shughuli mbalimbali za utalii na kutembelea vivutio vilivyopo mkoani humo.

Tamasha hilo lilianza Desemba 27 na kufungwa 28, Watanzania mbalimbali waliojitokeza walitembelea mapango ya asili ya Chaga Curve yaliyoko Marangu na Kibosho Kirima, ambako walitembelea mapango ya asili ya Nubi Curve.

Kwa mujibu wa Mmasi, licha ya mkoa huo kuwa na vivutio vingi, sio rahisi kwa siku moja kuvimaliza vyote na kwamba hatua hiyo ni sehemu ya kufungua njia kwa wakazi wa Kilimanjaro na Watanzania na wageni kutembelea vivutio mbalimbali vikiwamo vya asili vilivyopo maeneo mbalimbali ya mkoa huo.



Mbunge wa Jimbo la Hanang', mkoani Manyara, Samwel Hhayuma (wa tatu kushoto), akiwakabidhi maofisa usafirishaji wa mji mdogo wa Katesh dume la ng'ombe kwa ajili ya kusherehekea sikukuu ya Mwaka Mpya juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Misaada waathirika Hanang' kuimarisha usalama chakula

**Na Jaliwason Jasson,** HANANG'

SERIKALI imesema misaada ya mbegu za mazao ya chakula, inayotolewa na wadau wa kilimo hivi sasa kwa waathirika wa maafa ya maporomoko ya tope, mawe na magogo yaliyoporomoka kutoka Mlima Hanang', inalenga kuimarisha usalama wa chakula.

Katibu Tawala wa Wilaya hiyo (DAS), Athuman Likeyekeye, akizungumzia misaada hiyo, alisema mbegu hizo ni mahususi kwa ajili ya kuwawezesha kupanda mazao mbalimbali, kwa ajili ya kukabiliana na njaa na kujiwekea uhakika wa chakula, baada ya maafa hayo.

Likeyeke, alisema hayo jana katika Wilaya ya Hanang', mkoani Manyara wakati akipokea msaada wa mbegu ya SEEDCO kutoka kwa Meneja Mauzo wa mikoa ya Manyara, Singida na Dodoma. Kampuni hiyo ya SEEDCO, imekabidhi tani tano za mahindi ya mbegu, ambayo ni sawa na kilogramu 5,000.

"Nawashukuru sana SEEDCO kwa niaba ya Mkuu wa wilaya, kwa kutukimbilia. Na hiki mlichofanya sio kidogo, hata mngeleta kilogramu 10 tungewashukuru," alisema Likeyekeye.

Ofisa Kilimo wa Mkoa wa Manyara, Samweli Dahaye, alisema msaada huo na mingine inayotolewa na wadau, ni kwa ajili ya wakulima walioathiriwa na maafa hayo.

Dahaye alisema kila mkulima, atapata mbegu za kuanzia kilimo, akisisitiza kwa Wilaya ya Hanang', msimu ujao wanatakiwa kulima zaidi ya hekta 100,000 za mazao ya chakula, mahindi peke yake zitalimwa hekta 90,000.

Akikabidhi msaada huo wa mbegu za mahindi, Meneja huyo wa SEEDCO, Eliya Kituye, alisema wameamua kuutoa baada ya kuguswa na maafa yaliyotokea.

Kwa mujibu wa Kituye, kwa mbegu waliyowapatia wakifuta kanuni za kilimo inatoa gunia kati ya 40 mpaka 45 kwa ekari moja.

WENGI HAWAJUI!...

# ‘Pasta’ kijana ‘Mmarekani’, aliyetia fora mtoto wa mwanamuziki Lovy

**Na Adam Fungamwango**

“NAFURAHI kuwa nyumbani, watu wengi hawafahamu kuwa mimi na familia yetu tuliishi Dar es Salaam miaka mingi kidogo iliyopita, mimi ni mtoto wa Msasani, Mikocheni na Kinondoni. Wakati nilipofika hapa nchini, nikamwambia mchungaji wenzangu aliyenipokea kuwa anatamani sana vitumbua, nikamwambia nitafutie chipsi mayai, nimefurahi kuwa nyumbani.

Yalikuwa ni baadhi ya maneno ya mchungaji Lovy Elias Longomba akiongea kwa alipokuwa akitoa mahubiri yake Desemba 8 kwenye mkesha uliofanyika kwenye Viwanja vya Posta jijini Dar es Salaam.

Ni mchungaji aliyepata mapokezi makubwa sana hapa nchini pamoja na kufanyiwa mahojiano na vyombo mbalimbali vya habari mithili ya mtu yeyote maarufu duniani.

Mwonekano wake, mavazi na ujana aliokuwa nao ulikuwa ni kivutio kikubwa kwa watu wengi, akikusanya umati wa watu kila anapokwenda na vyombo mbalimbali vya habari, redio na televisheni vikitaka mahojiano naye.

Wengi walifahamu kuwa kwa sababu anatoka nchini Marekani, basi hawezi kuzungumza ligha ya Kiswahili.

Cha kushangaza alipotua tu Uwanja wa Ndege wa Mwalimu Julius Nyerere alitwanga Kiswahili kiasi cha kuwashangaza wengi kwa mchungaji, Mmarekani, mkazi wa Los Angeles kukitwanga kiswahili kama ametoka Mburahati, ilikuwa ni maajabu makubwa.

Alivuta vijana wengi kwenda kwenye mkutano wa Injili, huku baadhi wakitamka kuwa wamekwenda pale kwa sababu yake, wamezoea kuona wachungaji wengi watu wazima na wanavaa suti, lakini kwa Lovy ni tofauti.

Wajihi, mavazi, mwonekano, uliwafanya vijana wengi badala ya kwenda disco wakaenda kusikiliza neno la Mungu.

Kutokana hilo, wengi wakawa wanajiuliza Lovy ni mtu wa aina gani. Ametokea wapi? Kwa nini anafahamu kiswahili?

**Mtoto wa mwanamuziki Lovy Longomba**

Lovy si jina lake halisi. Anaitwa Elias Longomba, ni mtoto wa mwanamuziki wa zamani Lovy Longoma alikuwa mwimbaji na mtunzi wa Super Mazembe ya Kenya na African Sound Orchestra ‘Afriso Ngoma’, ya Tanzania, Lovy Longomba, iliyokuwa inamilikiwa na mfanyabiashara maarufu wakati huo, Juma Mwendapole.

Lovy, mwimbaji mwenye sauti nyembamba, nyororo alizaliwa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, na alivuma sana alipokwenda nchini Kenya na kujiunga na bendi ya Super Mazembe akiwa mwimbaji kiongozi.

Na huku ndipo alipomzaa mchungaji huyo, Novemba 25 mwaka 1986.

Kwa maana hiyo, Elias ni Mkenya kwa kuzaliwa, huku akiwa na asili ya DR Congo kwa baba yake Lovy na mama yake mzazi, Mado Zaina.



Mado Zaina alikuwa akiimbwa kwenye nyimbo mbalimbali na mumewe Lovy.

Kutokana na kufanana sana na baba yake, akapachikwa jina la Lovy, ambalo ndilo linalovuma hadi leo na yeye mwenyewe anapenda kulitumia zaidi kuliko Elias.

Mwaka mmoja baadaye, Lovy alikuja nchini Tanzania na familia yake kuliongoza kundi zima la Afriso Ngoma lililokuwa na maskani yake Msasani, Dar es Salaam.

Na huko ndiko Lovy alipokuwa akiishi na familia yake, akiwemo mchungaji Elias.

Baadaye walihamia Mikocheni, hadi pale Lovy alipondoka kwenye kundi la Afriso na kuunda kundi lake aliloliita Super Lovy Mokonyonyo, na makazi yao yakahamia Kinondoni, Dar es Salaam.

Hapo sasa unaweza kuona ni kwa nini mchungaji huyo alikuwa anazungumza kiswahili fasaha na kwa nini alisema Tanzania ni kama nyumbani.

Inawezekana kabisa Elias na ndugu zake wasingerejea kuishi nchini Kenya kama baba yao Lovy Longomba asingefariki dunia kwa ajili ya gari mwishoni mwa miaka ya 1989.

Mwanamuziki huyo alifariki maeneo ya Kambi ya Chokaa, Arusha wakati basi la abiria aina ya Takrim lilipogonga kwa nyuma lori lililokuwa limeharibika bila kuwekewa alama yoyote kwenye barabara kuu ikitokayo Dar es Salaam kwenda Arusha.

Lovy alikuwa akitokea nchini Kenya kuja Tanzania akiwa katika harakati zake za kimuziki, akiwa nakuja kuchukua baadhi ya wanamuziki wa Kibongo na kuwafanyia utaratibu wa pasipoti na visa baada ya kupata mkata wa kupiga muziki nchini Japan.

Ina maana siyo kuishi tu, hata baba yake mchungaji Elias Lovy alifia kwenye ardhi ya Tanzania na kuzikwa kwenye makaburi ya Lang’ata nchini Kenya.

Baada ya hapo yeye na ndugu zake na mama yao, Mado Zaina.

**Mwanamuziki na kundi la Longombas**

Kutokana na kuwa na damu ya muziki, watoto wa Lovy waliunda kundi walililolita, Longombas mwanzoni mwa mwaka 2000 nchini Kenya na kutikisa Afrika Mashariki nzima.

Liliundwa na yeye mwenyewe Elias Longomba, ambaye kwa sasa ni mchungaji, kaka yake Christian Longomba aliyefariki mwaka 2021 nchini Marekani alipokwenda kuuguzwa na mdogo wake.

Walipata tuzo nyingi kutokana na ngoma zao zilizotikisa mpaka nchini Tanzania kama ‘Dodosa’, ‘Poga Makofi’,’ Shika More’ na ‘Vuta Pumzi’.’

Mwaka 2007 kundi lilikwenda nchini Marekani, yeye akabaki huko, akaachana na mambo ya muziki wa dunia na kuanza kutumikia Mungu.

**Dada yake Elly Longomba**

Mchungaji Elias Longomba pia ni dada wa mnenguaji na mwimbaji wa zamani wa bendi ya Diamond Sound ‘Wanakimbinda Nkoi’, iliyotikisa nchini mwanzoni mwa miaka ya 2000, Elly Longomba.

Ina maana kuwa familia ya mwanamuziki Lovy iliyokaa Msasani, Mikocheni na Kinondoni ilikuwa ni ya watoto watato, Elias, Christian na Elly.

Elly, baada ya kutoka nchini alikwenda nchini Cameroon katika harakati za kusaka maisha kwa kazi yake ya muziki na alifariki akiwa nchini humo.

**Ndugu wa Awilo Longomba**

Mchungaji Elias Longomba vile vile ni ndugu wa mwanamuziki maarufu Afrika, Awilo Longomba.

Awilo na baba wa Mchungaji, Lovy wamezaliwa baba mmoja, mama mbalimbali.

Kwa maana hiyo, Elias anamwita Awilo baba yake mdogo, kwani Lovy alikuwa mkubwa kiumri.

**Babu yake ni mwanamuziki**

Msingi wa hayo yote ni mwanamuziki Vicky Longomba ambaye alikuwa pamoja na Franco kwenye bendi ya OK Jazz, baadaye akaanzisha bendi yake aliyoiita Lovy du Zaire miaka ya 1950 hadi miaka ya 1970 nchini Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

Huyu ndiye baba wa Lovy na Awilo akiwazaa kwa mama tofauti, na ndiye babu wa mchungaji Elias aliyekuja nchini hivi karibuni na kuwa gumzo.

**Tuma meseji 0716 350534**

HABARI KIMATAIFA

## Wapalestina ni purukushani usiku, mchana kujiokoa

**GAZA,** PALESTINA

WAKATI vikosi vya Jeshi la Israel vinazidi kusonga mbele kufika katikati ya ukanda wa Gaza, jumla ya Wapalestina 150,000 wanatakiwa kuondoka na kuelekea maeneo salama.

Umoja wa Mataifa ulisema idadi hiyo ya watu ni kubwa kutakiwa kuhama ili kupisha majeshi ya Israel kusonga mbele kuelekea kwenye kambi za wakimbizi zilizo katikati ya mji wa Gaza.

Baadhi ya mashahidi waliripoti kwamba vifaru vilikuwa vimefika kwenye viunga vya mashariki mwa kambi ya Bureij.

Jeshi la Israel hivi karibuni lilizidisha mashambulizi yake ya ardhini kulenga eneo la Bureij na kambi za jirani za wakimbizi za Nuseirat na Maghazi.

Wizara ya Afya inayoongozwa na Hamas, ilisema mashambulizi hayo ya mabomu yameua makumi ya watu ndani ya Gaza Alhamisi.

Vita hivyo vimetokana na shambulizi la kushtukiza ambalo limefanywa na Hamas kusini mwa Israel Oktoba 7, na kusababisha mauaji ya watu 1,200, huku wengine 240 wakichukuliwa mateka.

Mpaka sasa watu 21,300 wameuawa katika maeneo mbalimbali ya Gaza, wengi wao wakiwa watoto na wanawake wakati vita hiyo imefikia wiki 11 za mapigano.

Aidha, Jeshi la Israel (IDF) limetoa wito wa kuhama kwa wakazi karibu 90,000 wanaoishi Nuseirat na watu wengine 61,000 waliokimbilia eneo hilo baada ya makazi yao kushambuliwa kuelekea kusini mwa mji wa Deir al-Balah.

Hata hivyo, Umoja wa Mataifa umeonya kwamba watu hao hawana sehemu ya kwenda kwa sababu eneo la Deir al-Balah tayari limejaa. **BBC**

**Jeshi la Israel hivi karibuni lilizidisha mashambulizi yake ya ardhini kulenga eneo la Bureij na kambi za jirani za wakimbizi za Nuseirat na Maghazi.**

# Viongozi wa makanisa DRC wabaini kasoro za uchaguzi

**KINSHASA,** DRC

VIONGOZI wa makanisa nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo wameutaja uchaguzi mkuu uliofanyika Desemba 20 mwaka huu, kuwa una kasoro nyingi, lakini walishindwa kutoa tamko la pamoja kuhusu matokeo yanayoendelea kutangazwa.

Tume ya Uchaguzi (CENI) inaendelea kujumuisha kura na kutoa matokeo ambayo mpaka jana yalionyesha Rais Filex Tshisekedi, anaongoza kwa kupata asilimia 77 za kura zote.

Katika ripoti ya awali wananchi wengi waliisubiri, ujumbe wa uchunguzi wa Kanisa Katoliki na kiprotestanti nchini humo ulieleza uchaguzi huo ulijaa kasoro ikiwamo kuchelewa upigaji kura, vituo vya kupigia kura kufungwa na ukiukaji wa katiba kwa kuongeza muda wa upigaji kura.

Ripoti hiyo iliyokusanywa kutoka kwa waangalizi 25,000 wa uchaguzi waliotumwa katika vituo vyote vya kupigia kura nchi nzima, ilisema kulikuwa na visa 9,000 vinavyoonyesha hitilafu za upigaji kura.

Baadhi ya kasoro hizo zilizotajwa na waangalizi wa makanisa hayo ni kucheleweshwa kwa upigaji kura ambao kulisababisha watu wengi kutojitokeza kupiga kura. Ripoti hiyo ilisema ni asilimia 26 pekee ya vituo vilivyofunguliwa kwa wakati, huku asilimia kubwa ya mashine za kupiga kura hazikufanya kazi.

Ujumbe huo uligundua matukio mengi ya ukiukwaji wa taratibu za upigaji kura ambayo huenda yaliathiri uadilifu wa matokeo katika maeneo tofauti.

"Kwa kuzingatia mazingira ambayo upigaji kura ulifanyika, waangalizi wa makanisa Katoliki na kiprotenstanti wanaiomba Tume ya Uchaguzi CENI kuzipa imani pande mbalimbali zinazohusika katika mchakato huu. Wanatakiwa kutaja idadi ya vituo vilivyofunguliwa Desemba 20 na vile vilivyofunguliwa baada ya tarehe hiyo," ilisema taarifa hiyo.

Baada ya kutolewa kwa ripoti hiyo, msemaji wa serikali ya DRC, Patrick Muyaya, alisema matokeo ya uchaguzi hayatafutwa licha ya kuwepo kwa malalamiko kutoka kwa wagombea wa upinzani ambao wanataka uchaguzi kurudiwa.

"Sote tuligundua kuwa kulikuwa na matatizo. Kulikuwa na maeneo ambayo vituo vya kupigia kura vilichelewa kufunguliwa. Kulikuwa na maeneo ambayo mashine hazikufika kwa wakati, kwingine kulikuwa na matatizo ya mashine. Lakini hapa, lazima pia tutambue shauku kubwa ya Wacongo ambao walisubiri saa 10 hadi 12 kwenye foleni ili kupiga kura," alisema Muyaya.

Hata hivyo, ripoti ya waangalizi wa makanisa hayo ilieleza kwa kifupi kuwa yalithibitisha mgombea mmoja wa urais alikuwa akiongoza kwa kushinda zaidi ya nusu ya kura zilizohesabiwa, kulingana na hesabu yao wenyewe.

Tume ya uchaguzi inatarajiwa kutangaza matokeo ya mwisho ya urais Jumapili ya wiki hii kabla ya Mahakama ya Katiba kuidhinisha matokeo hayo Januari 10, mwakani. **DW**



Moja ya shambulio baya lililofanywa na Jeshi la Israel dhidi ya kambi ya wakimbizi ya Nur Shams katika Ukingo wa Magharibi. Pichani mtoto akipita katika kifusi cha jengo lililoteketezwa na mabomu hivi karibuni. **PICHA: REUTERS**

# Trump azidi kubanwa kuwania urais

**MAINE,** MAREKANI

RAIS wa zamani wa Marekani, Donald Trump, anaendelea kubanwa baada ya mahakama nyingine kumzuia kuwania nafasi ya urais wa nchi hiyo.

Katika hukumu iliyotolewa na Mahakama ya Jimbo la Maine, ilieleza kutokana na kushindwa kuzia shambulio la uvamizi katika jengo la bunge la Capitol mwaka wa 2021, hapaswi kuwania kinyang'anyiro cha urais.

Jimbo hilo ni la pili kutoa uamuzi unaolingana na kutafsiriwa kwamba jina la rais huyo wa zamani, ambaye sasa anafanya kampeni za kuchaguliwa na chama chake kupeperusha bendera katika uchaguzi utakaofanyika mwakani, jina lake haliwezi kuonekana kwenye karatasi za kupigia kura.

Akinukuu vifungu vya katiba vinavyohusiana na uasi huo, Shenna Bellows amebaini kwamba Donald Trump hapaswi kuwania nafasi hiyo kwenye uchaguzi kutokana na kuhusika na shambulio la Capitol Januari 6, 2021. Uamuzi huo ulifanywa baada ya kundi la wabunge wa zamani wa pande mbili kuhoji maoni ya Donald Trump kugombea katika Jimbo llinalotawaliwa na Chama cha Democratic.

"Hafai kuhudumu kama rais chini ya marekebisho ya 14 ya Katiba, ambayo hayajumuishi uwajibikaji wa umma wale ambao wamejihusisha na vitendo vya uasi, alisema Shenna Bellows katika hati rasmi ya serikali.

Hii ni mara ya pili ndani ya wiki mbili kwa Donald Trump kutangazwa kuwa hapaswi kuwania katika kinyang'anyiro cha urais kwa sababu hizo hizo.

Katika Jimbo la Colorado, Mahakama ya juu iliamuru kuondolewa kwa jina la rais wa zamani kwenye orodha ya wagombea katika jimbo hilo.

Uamuzi huo umekosolewa vikali na kambi ya bilionea huyo ambaye anatoka Chama cha Republican wakieleza ni ujanja unaotumika kuharibu uchaguzi.

Rais huyo wa zamani, anayepewa nafasi kubwa kushinda katika kura za mchujo za Chama cha Republican, anakusudia kupeleka suala hilo katika Mahakama ya Juu ya Marekani, ambayo itakuwa na jukumu la kuamua kama ataweza kuwania nafasi hiyo katika uchaguzi. **RFI**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

WAMILIKI WA KAMPUNI YA **NEYVICTORY LIMITED** YENYE NAMBA ZA **USAJILI 110554** ILIYOPO UBUNGO DAR ES SALAAM, INAYOJISHUGHULISHA NA BIASHARA YA UUZAJI WA VIFAA VYA MASHULENI WANAPENDA KUUTANGAZIA UMMA KUWA KAMPUNI YAO INATARAJIA KUFUNGWA NDANI YA SIKU CHACHE ZIJAZO KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI, KUTOKANA NA KUSHINDWA KUJIENDESHA YENYEWE.

HIVYO KWA YOYOTE MWENYE MADAI AU TAARIFA ZAIDI AFANYE MAWASILIANO NAO AU AFIKE OFISINI KWA MAELEZO ZAIDI.

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 27797 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE ALEX YOHANA MHYELA**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY BENJAMIN ALEX MHYELA**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 18th day of December 2023
Dated at Korogwe this 21st day of December 2023

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 27958 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE JULIANA ISARIA SHOO**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY MARTIN SAMSON NENGE**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 16th day of January 2024
Dated at Korogwe this 18th day of December 2023

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EMMANUEL JAMES LYIMO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA IPSUM yenye jina la umiliki VILLAGE SUPERMARKET LIMITED, USAJILI NAMBA: T 595 CSX, CHASSIS NAMBA: ACM215025042 na ENGINE NAMBA: 2AZ0712586. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/ILA/59604/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya Arumeru**
**Kituo cha Maji ya Chai**
**Mkoa Arusha**
**Usimamizi wa mirathi na 111/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU Eliuipa Godfrey Ngomuo WA Makumira**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA Amos Godfrey Ngomuo**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 15 Mwezi 01 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 28 Mwezi 12 Mwaka 2023

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
MAJI YA CHAI

**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT**
**(CAP.117)**
**CHANGE OF NAME BY DEEDPOLL**

BY THIS DEED, I, DINNAH ARIRA MNZAVA of P.O. BOX DAR ES SALAAM, DO HERBY wholly, absolutely and utterly renounce, relinquish and abandon the use of my former names of DINNAH HAROLD UISO and adopt as from the date of this deed poll and in substitution of my former name, the name of DINNAH ARIRA MNZAVA.
The reason for the changes of my names are that when I got married with my late husband I adopted the names DINNAH HAROLD UISO as it appears on my NMB account number 22601608816 but it's my wishes from now onward to subscribe the names of DINNAH ARIRA MNZAVA as it shows on most of my transactions including my citizen identity card number 19720818-14111-00001-12
For the purpose of evidence of such determination, I , hereby DECLARE that I shall at all times hereinafter in all records, deed, documents and other writings and in all action, suits and proceedings as well as in all public and private dealings and transactions and creations whatsoever use and subscribe the said name of DINNAH ARIRA MNZAVA as my name in lieu of and in substitution for my former names of DINNAH HAROLD UISO.
AND I HEREBY expressly authorize and require all and every person and whatsoever at all times after the date hereof to designate, describe and address me by the adopted name of DINNAH ARIRA MNZAVA.
IN WITNESS WHEREOF I have set my hand at Dar es Salaam, and I hereon substitute my old names of DINNAH HAROLD UISO by my new name of DINNAH ARIRA MNZAVA.

SIGNED and DELIVERED by the said DINNAH ARIRA MNZAVA
DEPONENT



## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOSEPH STEVEN MGUSI** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T-532 DCZ CHASSIS NO AZR600315303 ENGINE NO 1AZ4886573 AINA YA TOYOTA NOAH KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFIA KITUO CHA KARIBU CHA POLISI
**PQR/ARU/ARU/10347/2023.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**NGABWE MKAMBA WAZIRI PONDA** anatangaza kupotea kwa hati yake ya kusafiria yenye namba TAE347434 iliyotolewa makao makuu DAR ES SALAAM, PCO mwaka 2020. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIN/60827/2023**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

***Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701***

**KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTE KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI. TUPIGIE: +255 - 0677020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# AZAM FC: TUMEJIRIDHISHA UWEZO WA NAVARRO

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa klabu ya Azam FC umesema ulimfuatilia kwa kina na kujiridhisha na uwezo aliona mchezaji wao mpya Franklin Navarro na kuamua kumsajili.

Azam juzi ilitangaza kumsajili nyota huyo mwenye miaka 23 raia wa Colombia aliyekuwa akicheza ligi daraja la pili nchini humo na tayari ameungana na kikosi cha timu hiyo visiwani Zanzibar.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa habari wa klabu hiyo, Hashim Ibwe alisema hawana mashaka kabisa na uwezo wa mchezaji huyo na wanaamini atawasaidia kufikia malengo yao katika mashindano mbalimbali yaliyopo mbele yao.

Alisema mchezaji huyo amejiunga na timu visiwani Zanzibar jana na atakuwa sehemu ya mipango ya benchi lao la ufundi linaloongozwa na makocha Youssouph Dabo na Bruno Ferry katika michuano ya Mapinduzi inayoendelea visiwani humo.

"Mkataba wake ni siri kati yetu, mchezaji pamoja na mtu anayemsimamia hii ni kupunguza presha kwa nyota wetu, tunaimani na mchezaji huyu na hatutaki kumpa presha kulingana na rekodi yake aliyotoka nayo kwao," alisema Ibwe na kuongeza,

"Ubora wa mchezaji huyu kwanza anaweza kucheza nafasi nyingi ikiwamo kiungo mshambuliaji, winga wa pande zote na pia mshambuliaji wa kati, na hiyo ndio namba yake halisi, mchezaji anayetoka kwenye ligi ya Colombia ni ligi yenye daraja kubwa, ukiangalia kuna baadhi ya timu kutoka Afrika Kusini na mabara mengine Ulaya wanasajili kutoka nchini humo na sisi Azam FC safari hii tumeenda huko," alisema Ibwe.

Aidha, alisisitiza kuwa bado wanaendelea kufanya usajili kwa kuongeza wachezaji wengine wakiwa na lengo la kuongeza nguvu kwenye timu yao na wanatarajia hivi karibuni kushusha vifaa vingine ambavyo vitaenda visiwani humo kuunga na wenzao.

"Tunahitaji kufanya usajili mapema ili kuwahi katika mashindano ya Mapinduzi yaliyoanza hivi karibuni, huko watapata muda wa kuzoeana na kumpa nafasi mwalimu kuweka mipango yake sawasawa kabla hatujarejea kwenye michezo ya Ligi Kuu," alisema Ibwe.

Kuhusu michuano hiyo ya Mapinduzi, Ibwe alisema lengo lao kubwa ni kuhakikisha wanacheza hatua ya fainali na kuchukua ubingwa huo.




Mshindi wa Twende Zetu Ivory Coast Ki-VIP', Ally Kiseto (kushoto), kutoka Pwani akiwa ameshika runinga aliyoshinda katika droo ndogo ya wiki hii iliyofanyika Dar es Salaam juzi, kulia ni Mwakilishi wa Kampuni ya Tigo, Justine Lawena na Mwakilishi wa Kampuni ya Betika, Clinton Charles. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Coastal yamtema kiungo wa Simba

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Coastal Union imeendelea kuwaacha baadhi ya wachezaji wake kwa lengo la kutoa nafasi ya kukiboresha kikosi hicho kwa kusajili wachezaji wengine na safari hii wametangaza kuachana na kiungo wake Abdulswamad Kassim ambaye aliwahi kuichezea Simba kabla ya kutimkia kwa wagosi hao.

Taarifa iliyotolewa jana mchana na klabu hiyo inasema kuwa wameachana na wachezaji watatu akiwamo Abdulswamad aliyeichezea klabu ya Simba 2021, akitokea Kagera Sugar.

Wachezaji wengine waliopewa mkono wa kwaheri ni Yakubu Abdallah na Daudi Mbweni.

Kuachwa kwa wachezaji hao kunatimiza idadi ya wachezaji sita walioondoka kwenye timu hiyo kwa kipindi kifupi tangu kufunguliwa na dirisha dogo la usajili Desemba 16 linalotarajiwa kufungwa Januari 15, mwakani.

Wachezaji walioachwa awali ni Mapinduzi Balama, Juma Mahadhi na Fran Golubic.

Habari zinasema, Coastal Union inataka kujizatiti kwa kusajili wachezaji wa viwango vya juu kipindi hiki, huku ikitajwa kuwa kwenye mazungumzo na Salim Aiyee kutoka Mbuni FC inayocheza Ligi ya Championship, pamoja na mshambuliaji wa zamani wa Yanga, Fiston Abdulrazack raia wa Burundi ambaye kwa sasa anaichezea Sofapaka ya Kenya.

Akizungumza na gazeti hilo, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Abbas El-Sabri alithibitisha kuwa wapo kwenye mazungumzo na baadhi ya wachezaji na kama mambo yatakuwa vizuri watawatangaza hadharani.

"Siwezi kusema ndiyo au hapana kwa sababu tuko kwenye pilikapilika za usajili. Tunataka kuongeza wachezaji watakaotutoa hapa tulipo na kutupeleka mbele, kwa hiyo tunaongea na baadhi ya wachezaji, wale ambao tutamalizana nao tutawatangaza," alisema El Sabri.

Coastal ipo nafasi ya sita katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ikiwa na pointi 19 baada ya kucheza michezo 14 mpaka sasa.

## Simba Queens yaipangia mikakati Yanga Princess

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufanikiwa kuvuna pointi tatu kwenye mchezo wao uliopita dhidi ya Baobab Queens, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Juma Mgunda, ameweka wazi kuwa sasa wameanza mikakati ya kuhakikisha wanaibuka na ushindi kwenye mchezo wao ujao dhidi ya watani zao Yanga Princess, utakaochezwa Januari 3.

Simba juzi iliibuka na ushindi mnono wa mabao 5-2 dhidi ya Baobab Queens ikiwa ni mchezo wa raundi ya pili ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania uliochezwa kwenye uwanja wa Azam Complex, jijini Dar es Salaam .

Baada ya kukamilika kwa dakika 90, Kocha Mgunda alisema wamemaliza mchezo na Baobab Queens salama na hakukuwa na majeraha makubwa sana na kuwapongeza wachezaji wake kuendelea kupata alama tatu muhimu.

Hata hivyo, alisema licha ya ushindi huo mnono bado ameona mapungufu na ameanza kufanyia kazi mazoezini ili kuhakikisha wanaimarisha ubora wao kabla ya mchezo unaofuata.

"Kwangu kila mechi inakuwa na mipango yake, tumemaliza mchezo na Baobab Queens, mikakati inayofuata ni juu ya mchezo unaofuata dhidi ya Yanga, huu utakuwa na mipango yake mingine na tayari tunaenda kuianza mazoezini, yapo mapungufu madogo niliyoyaona, naenda kuyafanyia kazi," alisema Mgunda na kuongeza,

"Hii ni Derby, lazima tujipange vizuri, tunarudi kwenye uwanja wa mazoezi kwa lengo la kuhakikisha tunapata pointi tatu kwenye kila mechi ili kufikia malengo yetu msimu huu," alisema Mgunda.

Kwa upande wake, Nahodha wa Simba, Vivian Corazone alisema Ligi imekuwa ngumu lakini wanaendelea kujiandaa kwa kila mchezo kuhakikisha wanapata alama tatu kwenye kila mchezo ili kufikia malengo yao ya kutwaa ubingwa msimu huu.

Alisema baada ya ushindi wa juzi nguvu zao wanazielekeza katika mechi ya 'Derby' dhidi ya Yanga Princess.

"Ligi imekuwa ngumu na timu zote zimejiandaa vizuri, tunarudi uwanja wa mazoezi kujiandaa na mchezo wetu dhidi ya Yanga, lengo letu kuu ni kuchukua pointi zote tatu dhidi ya watani wetu," alisema Vivian.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### DE LIGT ANUKIA ARSENAL

ARSENAL wanavutiwa na mlinzi wa Bayern Munich ambaye ni raia wa Uholanzi, Matthijs de Ligt, mwenye umri wa miaka 24, ingawa kuna uwezekano wa makubaliano yoyote kufanyika msimu huu wa joto. **(Athletic)**

### NYOTA ARSENAL KUUZWA

KLABU ya Arsenal lazima iwauze wachezaji kabla ya kusajili katika dirisha dogo la usajili la Januari na Kocha, Mikel Arteta, huenda akatanguliza mikataba ya mkopo. **(Mirror)**

### COOPER ATAJWA CRYSTAL

MUSTAKABALI wa Roy Hodgson kama Kocha wa Crystal Palace hauna uhakika kwa sababu mabosi wa timu hiyo wanafikiria kumchukua, Steve Cooper, ambaye alitimuliwa na Nottingham Forest mwezi huu. **(Telegraph)**

### FIRMINO AGEUKA LULU

MSHAMBULIAJI wa Brazil, Roberto Firmino, mwenye umri wa miaka 32 anaweza kuondoka Al-Ahli baada ya miezi sita pekee, huku timu nyingine za Saudi Pro League zikiwamo Al-Shabab, Al-Ettifaq na Al-Fateh, Sheffield United na klabu za Uturuki zikimtaka. **(Sport)**

### GUIRASSY NJIA MOJA

MSHAMBULIAJI wa Guinea, Serhou Guirassy, mwenye umri wa miaka 27, yuko tayari kuondoka Stuttgart dirisha lijalo na AC Milan, Manchester United na Tottenham Hotspur zinavutiwa naye. **(Gazzetta dello Sport)**

### PHILLIPS KUONDOKA CELTIC

LIVERPOOL ipo tayari kumpeleka kwa mkopo mlinzi, Nat Phillips, mwenye umri wa miaka 26 katika timu nyingine kwenye dirisha la Januari baada ya muda wake wa kuitumikia Celtic kumalizika. **(Liverpool Echo)**

### EKWAH, EKITIKE SOKONI EPL

KLABU ya Crystal Palace inamtaka kiungo wa kati wa Sunderland mwenye umri wa miaka 21, Pierre Ekwah na mshambuliaji wa Ufaransa na Paris St-Germain, Hugo Ekitike (21). **(Standard)**

### LUKAKU, VLAHOVIC KITAELEWEKA

MKATABA wa kubadilishana unaohusisha mshambuliaji wa Juventus na Serbia, Dusan Vlahovic, mwenye umri wa miaka 23 na mshambuliaji wa Chelsea na Ubelgiji, Romelu Lukaku, ambaye yuko kwa mkopo AS Roma, unaweza kufanyika mwaka ujao. **(Tuttosport)**

### MARTINS ANUKIA FOREST

KLABU ya Nottingham Forest ipo katika mazungumzo ya juu na Monaco kuhusu kumnunua winga wa Timu ya Taifa ya Ureno, Gelson Martins, mwenye umri wa miaka 28. **(L'Equipe)**

### HOJBJERG KUTUA JUVENTUS

KLABU ya Juventus itaweka kipaumbele usajili wa kiungo wa kati kutoka Tottenham Hotspur na Timu ya Taifa ya Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg, mwenye umri wa miaka 28. **(Calciomercato)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA AKATAA KUILAUMU VAR

Ni baada ya timu yake kupokea kichapo kutoka kwa...

**LONDON, England**

MIKEL Arteta alikataa kulaumu tatizo la teknolojia kusababisha Arsenal kupokea kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa West Ham United, wakati walipoingia katika mzozo mwingine wa VAR kwenye mchezo huo wa Ligi Kuu England uliochezwa juzi.

Tomás Soucek alifunga bao la kuongoza dakika ya 13, lakini lilinusurika kukataliwa baada ya kukaguliwa kwa muda mrefu, huku ikionekana kama mpira ulitoka nje na Jarrod Bowen akaurudisha ndani kutengeneza pasi ya bao.

Bao hilo lililotolewa na mwamuzi, Michael Oliver, halikuwa na ushahidi wa kutosha kutoka kwenye kamera zilizopo ili kubaini kama ilitoka nje ya uwanja, sawasawa na tukio kama hilo ambalo lilishuhudiwa, Anthony Gordon, akifunga bao kwenye ushindi wa 1-0 wa Newcastle United dhidi ya wagonga nyundo hao Septemba, mwaka huu.

Arteta alipambana kwa mafanikio na FA baada ya kutoadhibiwa kwa maoni yake aliyoyatoa baada ya bao la Gordon.

Na baada ya mchezo wa juzi Arteta alionekana kutokosoa maamuzi ya VAR akisema timu yake ilikosa nafasi ya wazi ya kukwea kileleni mwa Ligi Kuu huku Konstantinos Mavropanos akiifungia West Ham bao la pili kwa kichwa dakika ya 55.

„Sijaiona, lakini wanasema teknolojia haijakamilika," alisema Arteta.

„Ni aibu kwa teknolojia tuliyonayo, ambayo haiko wazi ili tuseme ikiwa mpira ulitoka au upo ndani, imekamilika, imepita, hakuna tunachoweza kufanya kwa sasa.

„Ikiwa teknolojia tuliyonayo kwa sasa haitoshi kutupa jibu hilo, tunachopaswa kufanya ni kushinda mchezo kwa mabao. „

Arsenal walipiga mashuti 30 baada ya kugusa mpira mara 77 kwenye eneo la kisanduku la West Ham na kuweka rekodi ya timu kumiliki mpira kwa muda mrefu eneo hilo lakini ikashindwa kufunga tangu mwaka 2008.

„Ndivyo ilivyo," aliongeza Arteta. „Lazima tujaribu kuzalisha. Ikiwa hatutafunga kwa mashuti 30, basi lazima tufanye 50 au 60 kujaribu kufunga.

"Hilo ndilo jambo pekee. Siwezi kufikiria mchezo ambao tuna miguso zaidi kwenye sanduku, ubabe zaidi na hali ndogo kwa mpinzani dhidi ya timu nzuri kabisa ya West Ham. Hata hivyo, leo (juzi) haikutosha kushinda mchezo."

# HUGO LLORIS ANUKIA LIGI KUU MAREKANI

**LONDON, England**

KLABU ya LAFC iko katika mazungumzo ya kumsajili golikipa wa Tottenham Hotspur, Hugo Lloris kutua kwenye Ligi Kuu ya Soka Marekani (MLS), kwa mujibu wa ESPN.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37 yuko katika mwaka wa mwisho wa mkataba wake na Spurs na Kocha Ange Postecoglou hajamchezesha hata dakika moja.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, mpango huo umekamilika na kukubaliwa kabla ya kukamilishwa na kuna uwezekano hakutakuwa na ada ya uhamisho inayohusika.

Spurs ilimsajili Guglielmo Vicario kutoka Empoli kwa ada ya pauni milioni 17.2 Juni, mwaka huu na mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia haraka akajitambulisha kama kipa chaguo la kwanza la Postecoglou.

Lloris alikuwa huru kuondoka katika majira ya joto lakini alikataa ofa za Lazio, Nice na klabu za Ligi Kuu Saudi Arabia.

Kipa huyo wa zamani wa Ufaransa alijiunga na Spurs akitokea Lyon mwaka wa 2012 na baada ya 'vita' vifupi vya kutafuta nafasi ya kuanza katika timu hiyo akiwa na kipa Brad Friedel, alifanikiwa kuwa nambari namba moja katika timu hiyo ya London Kaskazini.

Lloris aliichezea Spurs zaidi ya mechi 400, akiteuliwa kuwa nahodha msimu wa 2015-16 na aliyekuwa kocha wa wakati huo, Mauricio Pochettino, kabla ya nafasi yake kuchukuliwa na Son Heung-Min muda mfupi baada ya Postecoglou kuchukua usukani.

Alitwaa Kombe la Dunia kama nahodha wa Ufaransa mwaka 2018 kabla ya kustaafu soka la kimataifa Januari, mwaka jana akiwa ameichezea mechi 145.



# Onana aomba kuchelewa AFCON

**MANCHESTER, England**

ANDRE Onana yuko katika mazungumzo na Chama cha Soka Cameroon ili kujaribu kucheleweshwa kujiunga kwake kwenye michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), kwa mujibu wa ESPN.

Kipa huyo wa Manchester United ameitwa katika kikosi cha Cameroon kuelekea michuano hiyo itakayoanza Januari 13, mwakani nchini Ivory Coast.

Onana, aliyesajiliwa kwa pauni milioni 43 majira ya joto kutoka Inter Milan ameonyesha atashiriki lakini, kwa mujibu wa ESPN anataka kupunguza muda wake nje ya Old Trafford kadri awezavyo.

Cameroon wanatarajiwa kushikilia kambi ya kujiandaa na mazoezi nchini Saudi Arabia, ambapo watacheza mechi ya kirafiki dhidi ya Zambia hapo Januari 9, mwakani.

Hata hivyo, Onana ana nia ya kuichezea United katika mechi ya raundi ya tatu ya Kombe la FA dhidi ya Wigan Athletic kwenye Uwanja wa DW hapo Januari 8, mwakani wakati Cameroon itaanza kampeni yake ya AFCON dhidi ya Guinea Januari 15.

Raundi ya mtoano itaanza Januari 27 huku fainali ikipangwa Februari 11, mwakani.

United wana mchezo wa Ligi Kuu England dhidi ya Tottenham Hotspur Januari 14, mwakani na uwezekano wa mechi ya raundi ya nne ya Kombe la FA mnamo Januari 27 na 28 kabla ya mechi za Ligi Kuu dhidi ya Wolves Februari Mosi. West Ham United Februari 4 na Aston Villa Februari 11, mwakani.

Onana alistaafu kucheza mechi za kimataifa wakati wa Kombe la Dunia nchini Qatar kabla ya kurejea Septemba, mwaka huu.

Pindi tu atakapojiunga na kikosi hicho cha Kocha Rigobert Song kwa ajili ya AFCON, Kocha Erik ten Hag, atalazimika kutoa mechi ya kwanza kwa kipa chaguo la pili, Altay Bayindir.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 hajaichezea United tangu kuhama kwake kutoka Fenerbahce majira ya joto, lakini aliichezea Uturuki wakati wa mapumziko ya mwisho ya kimataifa.

Ten Hag pia ana Tom Heaton mwenye umri wa miaka 37 kwenye kikosi chake.

# Zaha atemwa Ivory Coast

**ABIDJAN, Ivory Coast**

WINGA wa Galatasaray, Wilfried Zaha (31), hajaitwa na Kocha Jean-Louis Gasset, katika kikosi cha wachezaji 27 cha Ivory Coast kwa ajili ya michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON).

Mchezaji huyo alihamia katika Ligi Kuu Uturuki kutoka Crystal Palace mwishoni mwa msimu uliopita, ameichezea Ivory Coast mechi mbili pekee za kirafiki mwaka huu na kukosa mechi za kufuzu AFCON na mzunguko wa kwanza wa kufuzu kwa Kombe la Dunia mwezi uliopita.

Gasset amewajumuisha Serge Aurier wa Nottingham Forest, Ibrahim Sangare, na Willy Boly pamoja na kiungo wa kati wa Al-Ahli, Franck Kessie na winga wa Trapzonspor, Nicolas Pepe, ambaye anarejea baada ya kukosekana kwa mwaka mmoja.

Ismael Diallo wa Hajduk Split aliitwa kwa mara ya kwanza, huku Lazare Imani wa Union Saint Gilloise akiunda kikosi chake cha pili.

Washambuliaji Sebastien Haller wa Borussia Dortmund na Karim Konate wa RB Salzburg pia wapo kwenye kikosi hicho ambacho ni wenyeji, kitamenyana na Guinea-Bissau katika mchezo wa kwanza Januari 13, mwakani.

Pia watacheza dhidi ya Nigeria na Equatorial Guinea katika Kundi A.

Kikosi kamili:

Makipa: Yahia Fofana (Angers SCO), Badra Ali Sangare (Sekhukhune United) na Charles Folly (ASEC Mimosas)

Walinzi: Serge Aurier (Nottingham Forest), Wilfried Singo (AS Monaco), Obite Ndicka (AS Roma), Ousmane Diomande (Sporting CP), Odilon Kossonou (Bayer Leverkusen), Willy Boly (Nottingham Forest) na Ghislain Konan (Al-Fayha).

Viungo: Idrissa Doumbia (Al-Ahli Doha), Franck Kessie (Al-Ahli), Sangare (Nottingham Forest), Seko Fofana (Al Nassr), Jean Michael Seri (Hull City) na Lazare Amani (Union Saint Gilloise)

Washambuliaji: Nicolas Pepe (Trapzonspor), Max-Alain Gradel (Gaziantep), Simon Adingra (Brighton & Hove Albion), Karim Konate (RB Salzburg), Sebastien Haller (Borussia Dortmund), Oumar Diakite (Stade Reims), Jonathan Bamba (Celta Boga (Jecemie), Christian Kouame (Fiorentina) na Jean-Philippe Krasso (Belgrade)

# AZAM FC YAIPANIA CHIPUKIZI UTD LEO

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BAADA ya kushuhudia timu yake ikibanwa mbavu na Mlandege kwenye mchezo wa kwanza wa Kombe la Mapinduzi juzi, Kocha wa Azam FC, Brunno Ferry, amesema mchezo wao wa leo dhidi ya Chipukizi United ni lazima wasake ushindi kama wanataka kuendelea mbele kwenye michuano hiyo.

Kerry amesema wamejiandaa vizuri kuhakikisha wanaibuka na ushindi kwenye mchezo wa leo utakaochezwa uwanja wa Aman.

Alisema kutoka sare mchezo wao wa juzi dhidi ya Mabingwa watetezi, Mlandege FC kulitokana na baadhi ya wachezaji wake kutokuwa makini uwanjani. „Mchezo na Chipukizi naamini wachezajii wangu watabadilika, ni mchezo muhimu sana kwetu na lazima tupambane kupata ushindi ili kuweka hai malengo yetu ya kucheza fainali ya michuano ya mwaka huu," alisema Ferry.

Alisema mchezo wowote kwao ni muhimu kupata alama tatu hivyo matumaini yake ni kuona wachezaji wake wanarejea mchezoni ili kufanikisha mipango yao baada ya kulazimishwa matokeo ya 0-0 kwenye mchezo wa kwanza dhidi ya Mlandege.

"Kwetu kila mchezo ni muhimu kuhakikisha tunapata alama tatu, kwa sababu kila mashindano tunayoshiriki mipango yetu ipo katika kuhakikisha tunapata ushindi na kusonga mbele hivyo lazima mchezo wetu wa pili tufanye vizuri," alisema Ferry.

Aidha, alisema kuhusu wachezaji ambao hawakuwepo katika mchezo wao wa kwanza hana uhakika kama watakuwepo katika mchezo wao wa pili kutokana na baadhi yao kuwa na majeraha na wanasubiri ripoti ya daktari wa timu hiyo kujua wataanza kuwatumia lini.

Wakati kocha wa Azam akisema hivyo, kwa upande wake, kocha wa Chipukizi FC, Mzee Ali alisema anawaheshimu wapinzani wao kwa kuwa wana uzoefu mkubwa wa mashindano hayo lakini watatumia udhaifu wao kuwaadhibu na kupata pointi tatu muhimu.

Alisema ingawa Azam FC wana wachezaji wenye uzoefu na uwezo mkubwa lakini bado mapungufu ambayo wameyaona na watayatumia kuhakikisha wanapata alama tatu kwenye mchezo huo wa leo.

"Matarajio yetu ni kuhakikisha tunashinda na kupata alama tatu katika mchezo wetu wa pili, tunajua tunaenda kukutana na timu ngumu na yenye uzoefu mkubwa katika mashindano kama haya, lakini kuna udhaifu tumeuona kwao ambao ni siri yetu hivyo udhaifu huo ndio utatufanya tupate matokeo kwao", alisema Mzee Ali.

Katika kundi lao, timu zote zina pointi moja ambapo mbali na Azam kutoka 0-0 dhidi ya Mlandege, Chipukizi nao juzi walipata matokeo kama hayo dhidi ya Vital'O ya Burundi.

## Tabora, KMC zaongoza sare Ligi Kuu Bara

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Tabora United na KMC zinaongoza kwa kutoa sare nyingi zaidi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara hadi kufikia raundi ya 14 ya ligi hiyo.

Timu hizo zina sare sita mpaka sasa ikiwa ni idadi ya juu zaidi kuliko zingine, Tabora United ikiwa imecheza michezo 14 na KMC michezo 13.

Wakati timu hizo zikiwa na idadi kubwa ya sare, Yanga ndiyo timu pekee ambayo haijatoka sare hata mchezo mmoja wa Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa.

Kwa mujibu wa dawati letu la takwimu, Yanga inayoshika nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi inapointi 30 baada ya kucheza michezo 11, imeshinda michezo 10 na kupoteza mchezo mmoja.

Timu zinazofuatia kwa kutoka sare mara nyingi baada ya Tabora na KMC ni Singida Fountain Gate, Namungo na Prisons ambazo zote zimetoka sare mara tano.

Takwimu zinaonyesha kuwa Azam ndiyo timu iliyofunga mabao mengi mpaka sasa kwenye ligi, ikiwa imepachika mabao 35, ikifuatiwa na Yanga yenye mabao 30 huku Simba ikiwa imefunga mabao 23.

Yanga ndiyo timu iliyoruhusu mabao machache zaidi mpaka sasa ikiwa imefungwa mabao sita tu, timu ambayo imeonekana kuruhusu mabao mengi hadi sasa ni Mtibwa Sugar ambayo imepachikwa mabao 29 mpaka kufikia raundi hiyo na Kagera Sugar inaongoza kwa kuwa timu iliyofunga mabao machache zaidi ikiwa na mabao nane pekee.

Simba na Yanga ndio timu zilizopoteza michezo michache zaidi kila moja ikipoteza mchezo huku Mtibwa Sugar ikiongoza kwa kupoteza michezo mingi, imepoteza michezo 10.

## Mkazi Mbagala aibuka mshindi Jackpot

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Mbagala jijini Dar es Salaam, Jumanne Kape, juzi aliibuka mshindi wa bonasi ya Jackpot inayoendeshwa na kampuni ya Sportpesa na kukabidhiwa fedha Sh. milioni 8.1.

Kape ameibuka mshindi baada ya kutabiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 na kushinda bonasi hiyo.

Akizungumza katika hafla fupi ya kukabidhiwa fedha hizo, mshindi huyo alisema alianza kucheza michezo ya kubashiri na kampuni hiyo kwa zaidi ya mwaka mmoja.

„Nilianza kucheza na Sportpesa mwaka 2022, nimekuwa nikishinda kiasi tofauti kama laki tano, laki mbili, lakini huu ni ushindi wangu mkubwa, kuna rafiki yangu ndio alinishawishi kuanza kucheza na Sportpesa," alisema Kape.

Alisema kabla ya kuanza kubashiri mara nyingi huwa anaziangalia kwanza timu na kuzichambua ndipo uweka ubashri wake kwa timu anazoamini zinaweza zikampa matokeo mazuri.

Aidha, alisema moja ya sababu iliyomfanya kuanza kucheza na Sportpesa ni baada ya kuona kiwango cha bonasi kinachotolewa na kampuni hiyo ambacho ni kikubwa ukilinganisha na makampuni mengine ya kubashiri.

„Nashukuru sana, fedha hizi nilizopata, nitawekeza kwenye biashara yangu na pia zitanisaidia kwenye kuendeleza ujenzi wa makazi yangu," alisema Kape.

Kwa upande wake, Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa Kampuni hiyo, Sabrina Msuya, alimpongeza mshindi huyo na kuwaasa Watanzania waendelee kuiamini Sportpesa kwani nao wanaweza wakaibuka washindi siku moja.

„Niwakumbushe tu Watanzania kuwa tuna bidhaa zetu za Jackpot katikati ya wiki, Supa Jackpot na michezo ya Casino ambayo yote inatoa nafasi ya kuibuka mamilionea," alisema Sabrina.




Mshindi wa bonasi ya Jackport inayoendeshwa na Sportpesa, Jumanne Kape, akishika mfano wa hundi ya Sh. milioni 8.1 baada ya kutabiri kwa usahihi michezo 12 kati ya 13. **PICHA: SPORTPESA**

Michezo
Jumamosi Desemba 30, 2023
Nipashe

Arteta akataa kuilaumu VAR
UKURASA 21



# YANGA YATOA SABABU KUMSAJILI OKRAH

●●● Winga huyo wa zamani wa Simba atatambulishwa kesho Zanzibar kwenye ...




**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Klabu ya Yanga umesema ulimfuatilia winga wa Ghana, Augustine Okrah na kuona anafaa kwenye kikosi chao na hivyo kuamua kumsajili ili kukiongezea nguvu.

Yanga imemsajili nyota huyo wa zamani wa watani zao Simba kwa kumpa mkataba wa miaka miwili na anatarajiwa kutambulishwa rasmi kesho visiwani Zanzibar wakati wa mchezo wao wa kwanza wa Kombe la Mapinduzi dhidi ya Jamhuri kwenye Uwanja wa Amaan.

Nyota huyo tayari ameshawasili nchini na kujiunga na timu hiyo na atakuwa miongoni mwa wachezaji kwenye msafara wa timu hiyo inayotarajia kuondoka leo kuelekeza Zanzibar.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema usajili wanaoufanya ni wakuboresha kikosi chao kulingana na matakwa ya Kocha wao Miguel Gamondi na hata ujio wa Mghana huo umepitishwa na kocha wao huyo.

Alisema awali walipanga kumtambulisha mchezaji huyo jana, lakini Rais wa timu hiyo, Injinia Hersi Said ametaka akatambulishwe Zanzibar.

Kwa mantiki hiyo, Okrah sasa atatambulishwa katika mchezo wa kesho dhidi ya Jamhuri.

"Huyu mchezaji ni mgeni lakini mwenyeji tunatarajia kumtambulisha katika mchezo wetu wa kwanza, utambulisho wake utafunika ile shoo ya msanii Diamond aliyoifanya pale uwanja wa Amaan, tunafanya usajili kwa mapendekezo na maagizo ya kocha wetu, alitaka tusajili winga, tumemfuatilia Okrah na kocha mwenyewe amefanya hivyo na ndio sababu ya kumsajili," alisema Kamwe.

Aliongeza kuwa timu hiyo inatarajia kuondoka leo kuelekea Zanzibar huku wakiwa na dhamila ya kutwaa taji la ubingwa wa michuano hiyo na ndio sababu ya kwenda na kikosi kamili.

"Safari hii tumejipanga vizuri kwenda Zanzibar, tunaenda kuchukua ubingwa wa michuano hii, tumeshaona michezo minne mpaka leo (jana), sasa sisi Yanga tunaenda kuwafundisha soka," alisema Kamwe.

Mbali na Okrah, Yanga pia inatajwa kuwa kwenye mazungumzo ya mwisho ya kumsajili nyota wao wa zamani Simon Msuva ambaye kwa sasa hana timu.

# Simba SC yatamba rekodi Mapinduzi

**Na Adam Fungamwango**

HUKU wakitarajiwa kuondoka kesho kwenda Zanzibar kwenye michuano ya Mapinduzi Cup, Simba imesema inataka kuweka rekodi ya kuwa timu ya kwanza kutwaa ubingwa wa michuano hiyo baada ya uzinduzi wa uwanja wa Amaan.

Michuano ya mwaka huu ya Mapinduzi Cup iliyoanza juzi inafanyika kwenye uwanja wa Amaan ambao umefanyiwa maboresho makubwa na kuzinduliwa wiki hii na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi.

Akizungumza Dar es Salaam jana, Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema kuwa malengo ya klabu na Kocha Mkuu, Abdelhak Benchikha ni kutwaa ubingwa huo kwa sababu utakuwa ni wa kwanza baada ya kukarabatiwa uwanja mpya wa Amaan.

Ahmed amesema wamekaa na mwalimu na kumwambia umuhimu wa kuchukua kombe hilo, kwani utaendelea kuweka rekodi ya klabu hiyo kutwaa mara nyingi kombe hilo tangu kuanzishwa kwake.

Mnyama atang'oa nanga tarehe 31 (kesho) kuelekea Zanzibar kuanza kampeni yetu ya kutafuta ubingwa wa Kombe la Mapinduzi ndani ya uwanja mpya wa Amaan, wachezaji wote ambao hawajaitwa kwenye timu zao za taifa, watakuwa Unguja kwa ajili ya michuano hii.

"Unajua kwa ukubwa wa Simba ni lazima tukaweke rekodi katika uwanja mpya, uwanja wa Amaan umeboreshwa na kuwa wa kisasa zaidi, na sisi Simba tunataka kuwa klabu ya kwanza kutwaa ubingwa ndani ya uwanja mpya wa Amaan," alisema Ahmed.

Alisema kikosi cha timu hiyo kipo imara na tayari kwa ajili ya michezo hiyo huko kocha wao Benchikha akipanga pia kutumia michuano hiyo kuijenga zaidi timu yake kabla ya kurejea kwenye michezo ya Ligi Kuu ya mashindano ya klabu bingwa Afrika hatua ya makundi kusaka tiketi ya kutinga robo fainali.

Simba inatarajiwa kushuka uwanjani Januari Mosi kucheza dhidi ya Maafande wa Kujenga Uchumi (JKU) katika mechi yao ya kwanza ya Kundi B ya michuano hiyo ya Kombe la Mapinduzi.

Simba iko kwenye kundi hilo pamoja na timu ya Singida Fountaine Gate na APR ya Rwanda.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >